## VIGOGO WALIOPETA


Abdulaziz Abood - Morogoro Mjini


Christopher ole Sendeka-Simanjiro.


Livingstone Lusinde-Mvumi


Mrisho Gambo - Arusha Mjini.


Salma Kikwete-Mchinga.


Spika Job Ndugai-Kongwa.


Dk. Philip Mpango-Manyovu


Dk. Tulia Ackson - Mbeya Mjini


Prof Adolf Mkenda-Rombo


Prof. Joyce N.dalichako - Kasulu Mjini


Ummy Mwalimu-Tanga Mjini


Prof. Palamagamba Kabudi-Kilosa.

# Wamekatwa

**Na Waandishi Wetu**

WAMEKATWA! Ndivyo unavyoweza kusema baada ya Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi Taifa (NEC), kupitisha majina ya makada watakaopeperusha bendera ya chama hicho kuwania ubunge huku ikikata majina ya vigogo kadhaa wakiwamo waliongoza kura za maoni majimboni.

Miongoni mwa waliokatwa, wamo mawaziri, wateule wa Rais walioamua kuachia nafasi zao kwenda kuwania ubunge na waliokumbwa na kashfa mbalimbali zikiwamo tuhuma za rushwa.

Orodha ya wateule hao iliyotangazwa jana jijini hapa na Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Humphrey Polepole, haikuwa na majina ya vigogo kadhaa wakiwamo aliyekuwa mawaziri Dk. Harrison Mwakyembe na Angellah Kairuki pamoja na Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba.

**Ifuatayo ni orodha ya wateule wa CCM kwa majimbo yote nchini.**

**DAR ES SALAAM**

Mussa Zungu (Ilala), Josephat Gwajima (Kawe), Issa Mtemvu (Kibamba), Dk. Faustine Ndungulile (Kigamboni), Abbas Tarimba (Kinondoni), Jerry Slaa (Ukonga), Doroth Kilave (Temeke), Bonnah Kamoli (Segerea), Abdallah Chaurembo (Mbagala), Kitila Mkumbo (Ubungo).

**DODOMA**

Keneth Nolo (Bahi), Deo Dejembi (Chamwino), Livingstone Lusinde (Mvumi), Mohammed Moni (Chemba), Anthony Mavunde (Dodoma Mjini), Job Ndugai (Kongwa), Ally Makoa (Kondoa Mjini), Dk. Ashatu Kijaji (Kondoa Vijijini), George Simbachawene (Kibakwe) na George Malima (Mpwapwa).

**GEITA**

Tumaini Magesa (Busanda), Constantine Kanyasu (Geita Mjini), Joseph Musukuma (Geita Vijijini), Dotto Biteko (Bukombe), Dk. Medard Kalemani (Chato), Nicodemas Maganga (Mbogwe) na Hussein Amar (Nyang'alwe).

**IRINGA**

Jesca Msavatambangu (Iringa Mjini), Jackson Kiswaga (Kalenga), William Lukuvi (Isimani), Lazaro Nyamoga (Kilolo), Cosato Chumi (Mafinga Mjini), Exaud Kigahe (Mufindi Kaskazini) na David Kihenzile (Mufindi Kusini)

**KAGERA**

Stephen Byabato (Bukoba Mjini), Jason Rweikiza (Bukoba Vijijini), Frolent Kyombo (Nkenge), Innocent Bashungwa (Karagwe), Innocent Bilakwate (Kyerwa), Ndaisaba Luhoro (Ngara), Ezra Chiwelesa (Bihalamuro), Charles Mwijage (Muleba Kaskazini) na Oscar Kikoyo (Muleba Kusini).

**KATAVI**

Isack Kamwele (Mlele), Geophrei Pinda (Kavuu), Sebastian Kapufi (Mpanda Mjini), Anna Lupembe (Nsimbo) na Moshi Kakoso (Mpanda Vijijini).

**KIGOMA**

Profesa Joyce Ndalichako (Kasulu Mjini), Dk. Philip Mpango (Manyovu), Aloyce Kamamba (Buyungu), Atashasta Nditiye (Muhambwe), Kirumbe Ng'enda (Kigoma Mjini), Asa Makanika (Kigoma Kaskazini), Nashon William (Kigoma Kusini) na Augustine Hole (Kasulu Vijijini).

**PWANI**

Muharami Mkenge (Bagamoyo), Ridhiwani Kikwete (Chalinze), Twaha Mpembenue (Kibiti), Silvester Koka (Kibaha Mjini), Selemani Jafo (Kisarawe), Abdallah Ulega (Mkuranga), Omary Kipanda (Mafia), Mohamed Mchengerwa (Rufiji) na Michael Muakamo (Kibaha Vijijini).

**MOROGORO**

Godwin Kunambi (Mlimba), Abubakar Asenga (Kilombero), Abdulaziz Abood (Morogoro), Ahmed Shabiby (Gairo), Antipas Mgungusi (Malinyi), Innocent Kalogeres (Morogoro Kusini), Shaaban Taletale (Morogoro Mashariki), Jonas Vanzilad (Mvomero), Deniss Lazario Londo (Mikumi), Prof. Palamaganda Kabudi (Kilosa) na Salim Hasham (Ulanga).

**LINDI**

Ndulane Francis (Kilwa Kaskazini), Kasinge Ally (Kilwa Kusini), Zuberi Kuchauka (Liwale), Hamida Abdallah (Lindi Mjini), Salma Kikwete (Mchinga), Nape Nnauye (Mtama), Amandus Julius Chinguiye (Nachingwea) na Kassim Majaliwa (Ruangwa).

**MTWARA**

Mtenga Selemani (Mtwara Mjini), Hawa Ghasia (Mtwara Vijijini), Abdallah Chikota (Nanyamba), Katani Katani (Tandahimba), George Mkuchika (Newala Mjini), Maimuna Mtanda (Newala Vijijini), Geofrey Mwambe (Masasi), Issa Mchungahela (Lulindi), Cecil Mwambe (Ndanda) na Yahaya Mhata (Nanyumbu).

**MBEYA**

Atupele Mwakibete (Busokelo), Ally Jumbe (Kyela), Masache Kasaka (Lupa), Francis Mtega (Mbarali), Dk. Tulia Akson (Mbeya Mjini), Anthon Mwantona (Rungwe) na Oran Njeza (Mbeya Vijijini).

**NJOMBE**

Edwin Swale (Lupembe), Deo Sanga (Makambako), Deodatus Mwanyika (Njombe mjini), Festo Sanga (Makete), Dk. Festo Tugange (Wanging'ombe) na Kamonga Lazarius (Ludewa).

**SHINYANGA**

Pratobas Katambi (Shinyanga Mjini), Boniphace Butondo (Kishapu), Ahmed Salum (Solwa), Jumanne Kishimba (Kahama Mjini), Elias Kwandikwa (Ushetu) na Iddi Kasimu (Msalala).

**SONGWE**

Godfrey Kasekenya (Ileje), George Mwenisongole (Mbozi), Japhet Hasunga (Vwawa), David Silinde (Tunduma), Kodesta Sichalwe (Momba) na Philipo Mulugo (Songwe).

**RUKWA**

Josephath Kandege (Kalambo), Visenti Mbogo (Nkasi Kusini), Aeshi Hillaly (Sumbawanga Mjini), Deus Sangu (Kwela), Ally Kessy (Nkasi Kaskazini).

**SIMIYU**

Andrew Mathew (Bariadi), Saimon Songe (Busega), Njalu Silanga (Itilima), Mashimba Ndaki (Maswa Magharibi), Nyongo Haruni (Maswa Mashariki), Leah Komanya (Meatu), na Luhaga Mpina (Kisesa).

**KILIMANJARO**

Charles Kimei (Vunjo), Dk. Godwin Mollel (Siha), Prof. Aloyce Ndakidemi (Moshi Vijijini), Salasisha Mafue (Hai), Anne Kilango (Same Mashariki), Mathayo David (Same Magharibi), Profesa Adolf Mkenda (Rombo), Priscus Tarimo (Moshi Mjini) na Anania Tadayo (Mwanga).

**TANGA**

Januari Makamba (Bumbuli), Dk. Alfred Kimea (Korogwe Mjini), Timotheo Mzava (Korogwe vijijini), Jumaa Aweso (Pangani), Shaban Shekilindi (Lushoto) na Kwagila Ruben (Handeni mjini).

Wengine ni Marko Salu (Handeni vijijini), Omar Kigua (Kilindi), Ummy Mwalimu (Tanga Mjini), Rashid Shangazi (Mlalo), Hamis Mwijuma 'MwanaFA' (Muheza) na Dustan Kitandula (Mkinga).

**ARUSHA**

Mrisho Gambo (Arusha Mjini), Noa Moleli (Arumeru Magharibi), Dk. John Pallangyo (Arumeru Msharikí), Daniel Tilemai (Karatu), Dk. Steven Kiluswa (Longido), Fredrick Lowassa (Monduli) na William Olenasha (Ngorongoro).

**MANYARA**

Paulina Gekul (Babati Mjini), Daniel Silo (Babati Vijijini), Samwel Kadai (Hanan), Isai Paul (Mbulu Mji), Flatel Gregory (Mbulu Vijijini) na Christopher Ole Sendeka (Simanjiro).

**MARA**

Vedastus Manyinyi (Musoma Mjini), Profesa Sospeter Muhongo (Musoma Vijijini), Robert Maboto (Bunda Mjini), Boniface Getere (Bunda Vijijini), Charles Kajege (Mwibara), Jumanne Sagini (Butiama), Jaffary Chege (Rorya), Mwita Kembaki (Tarime Mjini), Mwita Waitara (Tarime Vijijini) na Dk. Jeresabi Mkimi (Serengeti).

**MWANZA**

Joseph Mkundi (Ukerewe), Dk. Angelina Mabula (Ilemela), Tabasamu Mwagao (Sengerema), Erick Shigongo (Buchosa), Stanslaus Mabula (Nyamagana), Alexander Mnyeti (Misungwi), Kasalali Mageni (Sumve), Shanif Mansour (Kwimba) na Bonaventura Kiswaga (Magu).

**SINGIDA**

Dk. Pius Chaya (Manyoni Mashariki), Yahya Massare (Manyoni Magharibi), Elibariki Kingu (Singida Magharibi), Miraj Mtaturu (Singida Mashariki), Mussa Sima (Singida Mjini), Mlali Ighondo (Singida Kaskazini), Francis Isack (Iramba Mashariki), na Dk. Mwigulu Nchemba (Iramba Magharibi).

**TABORA**

Nicolaus Ngassa (Igunga), Seif Gulamali (Manonga), Almasi Maige (Tabora Kaskazini), Venance Daudi (Igalula), Emmanuel Mwakasaka (Tabora Mjini), Hussein Bashe (Nzega Mjini), Dk. Hamis Kigwangalla (Nzega Vijijini), Seleman Zedi (Bukene), Aloyce Kwezi (Kaliua), Rehema Bigila (Ulyankulu), Magreth Sitta (Urambo) na Joseph Kakunda (Sikonge).

HABARI KITAIFA

# JPM: Haikuwa kazi rahisi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais John Magufuli (pichani), amebainisha namna ilivyokuwa ngumu kwa vikao vya juu vya chama kuchambua wagombea ubunge na uwakilishi kupitia chama hicho katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Amesema Kamati ya Usalama na Maadili na Kamati Kuu ya chama hicho vilitumia muda mrefu kuwajadili wagombea kutokana na kulazimika kutumia taarifa nyingi kutoka vyanzo mbalimbali kufanya uchambuzi wa kina wa makada wote 10,367 waliojitokeza. Rais Magufuli alitoa kauli hiyo jana alipofungua kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) kilichofanyika kwenye ukumbi wa Makao Makuu ya chama hicho jijini hapa.

Alisema vikao hivyo vililazimika kutumia taarifa nyingi na kuwajadili wagombea kwa muda mrefu, ili kupitisha wagombea wenye uwezo wa kupeperusha vyema bendera ya chama hicho na kukipatia ushindi mkubwa wakati wa uchaguzi.

"Ilitubidi tufanye uchambuzi wa kina kwa sababu wa unyeti wa nafasi wanazogombea. Kama mnavyojua, nafasi ya ubunge na uwakilishi ni nyeti na muhimu sana, ndiyo wasemaji wa wananchi, pia wana jukumu la kusimamia serikali. Hivyo basi ilikuwa ni lazima tujiridhishe kuwa tutakapowapitisha watakuwa na uwezo wa kutimiza majukumu hayo," alifafanua.

Alibainisha kuwa, majina ya wagombea yalijadiliwa kwenye vikao juzi, ngazi ya kamati ya usalama na maadili na kisha



kamati kuu ya ajili ya uchambuzi wa kina.

"Ninapenda niwahakikishie kuwa uchambuzi wa kina kweli kweli, tulitumia taarifa nyingi ambazo tulizitoa kutoka vyanzo mbalimbali na mimi ninapenda kuwathibitishia wajumbe, nimesoma majina yote 10,367.

"Uchambuzi wa kila mmoja wa kina tunao hapa na mabegi mengine yapo huku nyuma, haya hapa pamoja na lingine lipo pale. Kwa yule atakayetaka ufafanuzi wa mtu yeyote, atapewa ufafanuzi wa kina, lakini Kamati Kuu tulikaa na kujadili vizuri ndiyo maana tumetumia siku mbili ili kurahisisha kazi ambayo mtaifanya leo (jana)," alisema.

Rais Magufuli alisema kuwa kwa uchambuzi uliofanywa na vikao husika, hawatakuwa wamempendelea mtu au kumnyima mtu haki yake.

"Kama mnavyofahamu, miongoni mwa wabunge na wawakilishi ndiyo watakapopatikana Waziri Mkuu, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, lakini mawaziri na manaibu wao, Spika, Naibu Spika, wenyeviti kwa serikali zote mbili, hivyo ilitulazimu tuwajadili kwa kina ili tujiridhishe kuwa wale tutakaowapitisha, wana sifa zinazostahili kuwa viongozi na wanafahamu dira ya nchi na sera za chama," alisema.

Kiongozi huyo wa CCM alisema Kamati ya Usalama na Maadili pamoja na Kamati Kuu zimejitahidi kuchambua na kupata wagombea wenye sifa zinazohitajika, ikiwamo kupata wagombea wenye uwezo wa kuongoza, wazalendo, wenye kujitoa kwenye chama, wanaofahamu mahitaji ya wananchi, wenye utayari wa kuwatumikia wananchi na Watanzania wote na wenye kukubalika kwa wananchi.

"Halmashauri Kuu ya Taifa ndiyo imepewa jukumu la mwisho la kujadili na kuteua wagombea. Wito wangu kwenu, tujadili mapendekezo hayo kwa umakini mkubwa kwa kumtanguliza Mungu mbele na kwa kutanguliza maslahi ya chama na taifa letu, tusiweke mbele undugu, urafiki, ukanda au udini bali uwezo wa mtu kuongoza," alisema.

Awali, Rais Magufuli alibainisha kuwa jumla ya wanachama 43,461 wa CCM wamejitokeza kuwania ubunge, uwakilishi na udiwani.

"Wanachama wengi sana wamejitokeza na hii inatokana kwamba chama hiki wanakipenda, wana CCM 10,367 walijitokeza kuchukua fomu katika nafasi ya ubunge wa jimbo na viti maalum, nafasi katika Baraza la Wawakilishi ni 786, na udiwani kata na viti maalum ni 33,094.

"Haya ni mafanikio makubwa kwa chama chetu, walioomba vijana ni wengi sana, wafanyakazi, wakulima, wafugaji, wavuvi, kinamama, kinababa, wasomi, walemavu, viongozi wa NGO, wote waliomba CCM na hii inadhihirisha CCM ni chama kinachopendwa sana," alifafanua.

Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, alisema kikao kinatakiwa kufanya uteuzi wa mwisho wa wagombea wa CCM wa nafasi za ubunge na uwakilishi kwa ajili ya uchaguzi mkuu 2020, lakini kutokana na ratiba za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kupishana, hakutafanyika uteuzi wa wawakilishi.

Alisema kikao kilitakiwa kuwa na wajumbe 167. Kati yao, 54 hawakuhudhuria kutokana na sababu za kikanuni kwamba wamegombea ubunge na uwakilishi.

"Kati ya hawa, 54 waliogombea ubunge ni 42 na uwakilishi ni 12, kwa hiyo, wajumbe wenzetu 54 hawawezi kushiriki kwenye uteuzi wetu kwa kuwa kanuni yetu inasema ukishagombea katika hatua ya uteuzi wa nafasi unayogombea, huwezi ukawa sehemu ya wajumbe wanaofanya uteuzi," alisema.

# Sura mpya zatawala ubunge CCM



Deo Ndejembi



Masache Kasaka

**Na Salome Kitomari**

SURA mpya jana zilitawala kwenye majina ya wanachama watakaopeperusha bendera ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika nafasi za ubunge utakaofanyika Oktoba, mwaka huu.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) Itikadi na Uenezi wa CCM, Humphrey Polepole, akitangaza majina ya walioteuliwa, alisema jana kuwa chama hicho kimeamua kuchanganya makundi yote wakiwamo wasanii na hasa kuangalia vijana umri wa miaka 30 hadi 40.

Katika uteuzi huo sura mpya zilizojotokeza ni Mfanyabiashara na Mmiliki wa Global Media, Erick Shigongo, ambaye atapeperusha bendera ya CCM katika Jimbo la Buchosa.

Aidha, katika Jimbo la Vunjo ameteuliwa aliyewahi kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Dk. Charles Kimei, ikiwa ni mara ya kwanza kutokeza katika medani za siasa. Jimbo la Kawe, aliyeshika nafasi ya tatu, Kiongozi wa Kanisa la Ufufuo na Uzima, Josephat Gwajima, ameteuliwa kupeperusha bendera ya chama hicho. Katika kura za maoni za jimbo hilo, mshindi alikuwa Furaha Dominic (101), Angella Kizigha (85) na Gwajima kura (79).

Sura mpya nyingine ni aliyepitishwa mwanamuziki wa kizazi kipya, Hamis Mwijuma maarufu kama Mwana FA atakayepeperusha bendera ya CCM katika Jimbo la Muheza. Mbunge wa jimbo hilo alikuwa Balozi Adadi Rajabu ambaye aliwahi kuwa Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI).

Msanii mwingine aliyeteuliwa ni Hamisi Taletale, maarufu kama Babu Tale ambaye atagombea Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki. Babu Tale ni Mkurugenzi wa Wasafi Media na alimshinda Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba.

Frederick Lowassa, mtoto wa Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, aliyeshinda kura za maoni Jimbo la Monduli, amepitishwa kugombea katika Jimbo la Monduli ambalo lilikuwa chini ya baba yake tangu mwaka 1995 kabla ya kujiengua CCM mwaka 2015 na kujiunga na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na kugombea urais kupitia vyama vilivyokuwa vikiunda Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA).

Sura zingine mpya zilizochomoza ni aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Iringa, Jessica Msambatavangu ambaye anagombea Iringa Mjini na Makamu wa Rais wa kampuni ya madini ya Barick Gold, Deo Mwanyika, aliyeteuliwa kugombea Njombe Mjini.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

UCHAGUZI WA RAIS NA WABUNGE WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NA MADIWANI TANZANIA BARA

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 utafanyika siku ya Jumatano tarehe 28 Oktoba, 2020. Ratiba ya mchakato wa Uchaguzi Mkuu ni kama ifuatavyo:-

| NA | TUKIO | TAREHE | MAHALI |
|---|---|---|---|
| 1. | Fomu za **UTEUZI** kwa Wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais | Kutolewa kuanzia tarehe 05 Agosti, 2020 hadi 25 Agosti, 2020 | Katika Ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Njedengwa, Jijini Dodoma |
| 2. | Fomu za **UTEUZI** kwa Wagombea Ubunge | Kutolewa kuanzia tarehe 12 Agosti, 2020 hadi 25 Agosti, 2020 | Katika Ofisi za Halmashauri husika |
| 3. | Fomu za **UTEUZI** kwa Wagombea Udiwani | Kutolewa kuanzia tarehe 12 Agosti, 2020 hadi 25 Agosti, 2020 | Katika Ofisi za Kata husika |
| 4. | **UTEUZI** wa Wagombea Kiti cha Rais na Makamu wa Rais, Ubunge na Udiwani | Utafanyika tarehe 25 Agosti, 2020 | Kwa wagombea Kiti cha Rais na Makamu wa Rais Ofisi za Tume Dodoma, Kwa wagombea Ubunge Ofisi za Halmashauri husika na kwa wagombea Udiwani Ofisi za Kata husika |
| 5. | Kampeni za Uchaguzi | Zitaanza tarehe 26 Agosti, 2020 hadi 27 Oktoba, 2020 | Maeneo yaliyopangwa kwa mujibu wa ratiba |
| 6. | Siku ya Uchaguzi | Itakuwa ni Jumatano tarehe 28 Oktoba, 2020 | Vituo vya kupigia kura |

SHIME MWANANCHI JITOKEZE KUMCHAGUA RAIS, MBUNGE NA DIWANI WAKO
KURA YAKO SAUTI YAKO NENDA UKAPIGE KURA

Gerald G. J Mwanilwa
Kny; MKURUGENZI WA UCHAGUZI

TUFUATILIE KUPITIA MITANDAO YA KIJAMII;-
Facebook: Tume Ya Uchaguzi-tz, Instagram: tumeyauchaguzi_tanzania
Twitter: Tume ya Uchaguzi-TZ, NEC TV: NEC ONLINE¬ TV

Tangazo hili limetolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi S. L. P 10932 Dar Es Salaam, Tel. +255 22 2114963-6. Nukushi: +255 22 2113382. Barua Pepe: info@nec.go.tz. Tovuti: www.nec.go.tz.

# Waliounga mkono juhudi wapeta

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HALMASHAURI Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Taifa (NEC), imewateua kuwania ubunge makada tisa waliokuwa wabunge kupitia vyama vya upinzani katika Bunge lililopita kisha kuhamia CCM.

Makada hao ni waliojiunga na CCM kutokana na kile walichodai kuunga mkono juhudi za maendeleo zinazofanywa na Rais John Magufuli na serikali yake.

Akitangaza majina ya walioteuliwa kuwania ubunge kupitia chama hicho jana jijini hapa, Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Humphrey Polepole, alisema kikao hicho kimemteua Pauline Gekul kuwania ubunge wa Babati Mjini.

Katika Bunge la 11, Gekul alikuwa mbunge wa jimbo hilo la Mkoa wa Manyara kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Polepole pia alisema Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, ameteuliwa kuwania ubunge wa Siha mkoani Kilimanjaro. Dk. Mollel alishinda ubunge wa jimbo hilo mwaka 2015 kupitia CHADEMA.

Wengine waliopenya kwenye orodha hiyo ya wateule ni Zuberi Kuchauka aliyeteuliwa kuwania ubunge wa Liwale mkoani Lindi. Kuchauka alishinda ubunge wa jimbo hilo mwaka 2015 kupitia Chama cha Wananchi (CUF).

NEC kupitia imempitisha Naibu Waziri Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Mwita Waitara, kuwania ubunge wa Tarime Vijijini. Mwaka 2015, Waitara alichaguliwa kuwa ubunge wa Ukonga jijini Dar es Salaam kupitia CHADEMA.

Katani Katani, ambaye katika Bunge la 10 alikuwa Mbunge wa Tandahimba (CUF), ameteuliwa kuwania ubunge wa jimbo hilo kupitia CCM alikotua hivi karibuni.

Vilevile, Cecil Mwambe, aliyetangaza kung'oka CHADEMA baada ya kushindwa katika uchaguzi wa kumsaka mwenyekiti wa chama hicho taifa, ameteuliwa na NEC kuwania ubunge wa Ndanda alikokuwa mbunge kupitia CHADEMA Bunge lililopita.

David Silinde, aliyekuwa Mbunge wa Momba (CHADEMA), amepitishwa na NEC kuwania ubunge wa Tunduma kupitia CCM.

NEC pia imewapitisha Joseph Mkundi na Ahmed Juma Ngwali kuwania majimbo ya Ukerewe mkoani Mwanza na Ziwani, Zanzibar, mtawalia. Mkundi alikuwa kada wa CHADEMA wakati Ngwali alikuwa mwanachama wa CUF na wote walishinda ubunge kupitia vyama hivyo mwaka 2015.



Ahmed Juma Ngwali - Ziwani



Dk. Godwin Mollel- Siha



Joseph Mkundi- Ukerewe.



Pauline Gekul-Babati Mjini



Katani Katani- Tandahimba



Mwita Waitara- Tarime Vijijini



Zubeir Kuchauka - Liwale



Silinde David - Tunduma

# Mawaziri, vigogo maarufu waenguliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BAADHI ya mawaziri na vigogo mbalimbali wameachwa katika uteuzi wa wagombea wa ubunge uliofanywa na Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), hivyo kuzima ndoto zao za ubunge katika uchaguzi mkuu mwaka huu.

Kikao hicho kilifanyika jana na kuteua majina ya wagombea wa ubunge wa majimbo na ubunge wa viti maalum, huku wengine wakikosa kuteuliwa licha ya kuonekana kuongoza kwenye mchakato wa kura za maoni. Akitangaza majina ya wagombea hao jana, Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Humphrey Polepole, alisema katika Jimbo la Kyela ambalo Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alikuwa mbunge na alianguka kwenye kura za maoni, ameteuliwa Ali Anyigulile Jumbe.

Aidha, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) ,Angellah Kairuki, alianguka mapema katika mchakato wa kura za maoni Same Magharibi. Aliyeongoza katika kura hizo, Dk. David Mathayo, ameteuliwa kugombea tena kwa mara ya nne mfululizo.

Katika Jimbo la Morogoro Mashariki, aliyekuwa Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, hayumo katika orodha ya walioteuliwa baada ya kushindwa katika kura za maoni. Aliyeteuliwa ni Meneja wa Msanii Daimond Platnumz, Hamisi Taletale.

Kigogo mwingine ambaye ameenguliwa kugombea kupitia Viti Maalum ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, licha ya kuongoza kura za maoni katika Mkoa wa Mbeya.

Mbali na hao, aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, hajapata fursa ya kuteuliwa kugombea Jimbo la Mwibara baada ya kuteuliwa Charles Kajege, ambaye aliwahi kuwa mbunge katika jimbo hilo mwaka 2005 hadi 2010. Lugola na Kajege walifungana katika kura za maoni.

Aidha, aliyewahi kuwa Waziri wa Kilimo, Dk. Charles Tizeba, hajateuliwa kugombea Jimbo la Buchosa na aliyeteuliwa ni Erick Shigongo, ambaye alifungana kura na Tizeba. Shinyanga Mjini, aliyekuwa Mbunge wa Shinyanga Mjini ambaye aliongoza kura za maoni Stephen Masele pia amekosa fursa hiyo.

NEC pia haijamteua aliyekuwa Mbunge wa Mbinga, Sixtus Mapunda, licha ya kuongoza kura za maoni. Pia aliyekuwa Mbunge wa Kigoma Kaskazini, Peter Serukamba, hajateuliwa na badala yake ameteuliwa Asa Makanika.

Aliyekuwa Mwenyekiti wa Bunge, Andrew Chenge, hajapenya katika mchakato wa kugombea Jimbo la Bariadi. Mwanasiasa mwingine maarufu ambaye ameenguliwa ni Waziri wa zamani wa Nishati na Mdini, William Ngeleja. Vigogo wengine ni aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, Mkuu wa Mkoa wa zamani wa Tabora, Aggrey Mwanri, mwanasiasa mkongwe Profesa Juma Kapuya na Amos Makala, ambaye aliwahi kuwa mkuu wa mkoa katika mikoa ya Kilimanjaro, Mbeya na Katavi

Halima Bulembo ambaye aligombea tena ubunge kupitia kundi la vijana licha ya kushika nafasi ya pili kwenye kura za maoni, hajateuliwa na NEC.

# Wateule wa JPM waliong'ara

**Na Augusta Njoji,**

**DODOMA**

WATEULIWA wa Rais John Magufuli waliokuwa kwenye nafasi mbalimbali, wameonekana kung'ara katika uteuzi wa wagombea ubunge watakaopeperusha bendera ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), katika uchaguzi mkuu mwaka huu.

Majina ya walioteuliwa kugombea ubunge na kutangazwa jana na Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi CCM Taifa, Humphrey Polepole, walipitishwa kwenye kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC).

Miongoni mwa wateuliwa hao ni aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Patrobas Katambi, ambaye atagombea Jimbo la Shinyanga Mjini na aliyekuwa Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, ambaye atagombea Jimbo la Mlimba.

Wengine ni aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Deogratias Ndejembi, atakayegombea Jimbo la Chamwino aliyekuwa Katibu Mkuu wa Maliasili na Utalii Prof. Adolf Mkenda.

Pia katika uteuzi huo, aliyekuwa Mkurugenzi wa Kituo cha Uwekezaji (TIC), Geoffrey Mwambe, ameteuliwa kugombea Jimbo la Masasi, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, atagombea Jimbo la Misungwi, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, atagombea Jimbo la Arusha Mjini na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Christopher Ole Sendeka, atagombea Jimbo la Simanjiro.

Aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu, Jumanne Sagini, atagombea Jimbo la Butiama, aliyekuwa Katibu Tawala Wilaya ya Rombo, Aboubakar Asenga, atagombea Jimbo la Kilombero na aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mvomero, Florent Kyombo, atagombea Jimbo la Nkenge.

# IGP Sirro aanika sababu za akaunti THRDC kufungwa

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi nchini limeeleza sababu za kufungiwa kwa akaunti za Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), kuwa ni kuchunguzi zaidi ya Sh. bilioni 6 zilizoingia kuanzia Januari mwaka 2019 hadi sasa.

Akizungumza na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), alisema Agosti 2, mwaka huu, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta wa Polisi (IGP) Simon Sirro, alisema alipata taarifa kuhusu miamala mingi inayoingia kwenye akaunti ya mtandao huo na kuanza ufuatiliaji.

"Kitengo chetu cha ufuatiliaji wa fedha haramu, walifuatilia benki na kubaini kuna fedha nyingi zimeingia benki kwa kipindi cha Januari 2019 hadi Agosti mwaka huu, Sh. bilioni 6 ziliingia kwenye akaunti za THRDC," alisema.

Sirro alisema polisi wanafanya uchunguzi kujua kama fedha hizo ni halali au haramu, na kama hazijaja kwa nia ovu.

"Tumekusanya nyaraka zote za fedha hizo na tunafanya mahojiano. Kwa mujibu wa kanuni zilizopo, Jeshi la Polisi lina mamlaka ya kusimamisha akaunti isifanyekazi kwa ajili ya uchunguzi kwa siku 14, na baada ya hapo kama tutaendelea na uchunguzi tutakwenda mahakamani ili watoe amri ya kuendelea kufunga hizo akaunti," alisema.

Aidha, Sirro alisema kwa sasa kuna changamoto ya ugaidi na kwamba Jeshi la Polisi linafuatilia kwa karibu kwa kuwa upo uwezekano wa fedha haramu kuingia nchini na kuchafua amani.

Kwa mujibu wa IGP Sirro, kinachotafutwa ni kuona uhalali wa miamala ya hizo fedha, kwa kujiridhisha kama ni halali zimekuja kufanya kazi gani ambazo ni halali.

"Tunafanya uchunguzi tukiona ni halali na zimekuja kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu hatuna tatizo...tumefungua jalada za uchunguzi kujua ni jinai au waliotupa taarifa kuna fitina fulani," alisema.

Pia, alithibitisha kuhojiwa kwa Mratibu wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, na kwamba kukiwa na kosa la jinai akaunti zitafunguliwa na kama hakuna wataruhusiwa kuendelea na shughuli zao.

Alipouliza kuhusu ulazima wa kufunga akaunti huku watu hawajalipwa mishahara, alisema: "Tukiruhusu wachukue hizo fedha kielelezo kitakuwa kimepotea, kesi haitasimama."

Olengurumwa alikamatwa na kuhojiwa wiki iliyopita na jana, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kilitoa tamko la kushtushwa na taarifa za THRDC kusitisha shughuli zake kufuatia kufungwa kwa akaunti zake.

"Tunatoa pole kwa Bodi ya Wakurugenzi, Mtaribu, wanachama wa THRDC kwa usumbufu wanaopitia katika kipindi hiki, LHRC tunaamini mamlaka husika zitalishughulikia suala hili kwa haraka ili kuuwezesha mtandao huo kuendelea na shughuli zake," ilieleza taarifa iliyotolewa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji, Fulgence Massawe.

Juzi Bodi ya Wakurugenzi ya THRDC, ilitoa taarifa kwa umma ya kusitisha shughuli zake zote kutokana na kushikiliwa kwa akaunti zake.

# Bangi magunia 116 yawaweka matatani tena vigogo Arumeru

**Na Daniel Sabuni, ARUSHA**

SHEHENA ya bangi iliyokuwa kwenye magunia 116, imekamatwa wilayani Arumeru mkoani Arusha na kuwaweka mtegoni tena viongozi wa wilaya hiyo.

Mtuhumiwa mmoja pekee, Kanael Akyoo (50), ametiwa mbaroni na kikosi maalum cha kupambana na dawa za kulevya, akidaiwa kukutwa na magunia matatu na viroba tisa vya bangi nyumbani kwake.

Julai 6 mwaka huu, Rais John Magufuli aliagiza kuondolewa kazini na kushushwa vyeo kwa aliyekuwa Mkuu wa Polisi Wilaya ya Arumeru (OCD), Ofisa Usalama wa Wilaya hiyo (DSO), Mkuu wa Upelelezi wa Wilaya hiyo (OC CID) na maofisa wengine wa vyombo vya ulinzi na usalama wanaohusika, baada ya kushindwa kudhibiti dawa hizo hadi Kaimu Kamishna wa Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya alipokwenda wilayani huko kufanya operesheni.

Jana, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini katika Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Florence Khambi, alisema bangi hiyo ilikamatwa katika Kitongoji cha Karafia kilichoko eneo la Kisimiri Chini wilayani Arumeru.

Kwa mujibu wa Khambi, operesheni hiyo iliongozwa na Kamishna Jenerali wa DCEA, James Kaji, kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi mkoani Arusha.

Alisema kuwa katika ukaguzi wa awali kwenye maeneo ya mashamba ya kitongoji hicho walifanikiwa kukamata magunia 116 ya bangi.

Alisema pamoja hayo, pia walikamata viroba tisa vya bangi, gunia 1 la mbegu na misokoto 714 ya bangi.

Alisema kuwa katika operesheni hiyo, pia walifanikiwa kumkamata mtuhumiwa mmoja Kanael Akyoo (50), mwanamke mkazi wa Karafia Kisimiri Chini akiwa na magunia matatu na viroba 9 vya bangi vikiwa vimehifadhiwa ndani ya nyumba yake.

"Juhudi za intelijensia ya taasisi hizo zilifanikisha kumkamta mtuhumiwa huyo na kwa kweli ni jambo jema, maana unapokamata kitu bila mtu inafikirisha," alisema.

Alibainisha kuwa magunia mengine 113 yalikamatwa katika nyumba zaidi ya 20 za wakazi wa eneo hilo ambapo watuhumiwa waliokuwa wakiyamiliki, walikimbia makazi yao.

Alisema kuwa mtuhumiwa Akyoo anatarajiwa kufikishwa mahakamani hivi karibuni baada ya mchakato wa upelelezi kukamilika.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, akizungumza na Nipashe jana kuhusiana na tukio hilo, alisema kuwa kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali vya udhibiti wa dawa za kulevya, wameendelea kupambana na biashara hiyo haramu wilayani huko na hivi karibuni walifanikiwa kukamata watu watano wakituhumiwa kujihusisha na biashara hiyo na tayari wameshafikishwa mahakamani.

Alisema kuwa jana walipanga kufanya ziara ya kikazi katika maeneo ya Kitongoji cha Karafia na vijiji vingine wilayani humo ili kutoa elimu na kubadili fikra za wananchi kuhusu kilimo cha bangi ambacho alidai wananchi wa huko wanaona ndiyo kipato cha kuendeshea maisha yao.

"Tutaambatana na wataalamu wa elimu za kilimobiashara, tuna programu ya kuelimisha kilimo cha pareto ambacho hustawi sehemu za baridi ambacho kina kipato zaidi ya kilimo na biashara haramu dawa za kulevya aina ya bangi. Kilo moja ya pareto ni Sh. 1,600 hadi 2,000. Kwa hiyo, kwenye gunia moja ni pesa nzuri kabisa na watabadilisha maisha yao na kuepuka bangi ambayo kila siku inawakutanisha na mkono wa dola," alisema Muro.


TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC — TACOBA — "Our Bank for Our Development"

**Mwenyekiti na Wanahisa,**

## Yah: Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa

Taarifa inatolewa kwamba Mkutano **Mkuu wa SITA wa Wanahisa wa Tandahimba Community Bank** utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 12 Septemba, 2020, katika **Ukumbi wa Maghala ya Chama cha Ushirika Tandahimba na Newala (TANECU), Tandahimba** kuanzia saa tatu kamili **(Saa 3.00) asubuhi** kujadili dondoo zifuatazo:

1. **Kufungua Mkutano.**
2. **Kuridhia Dondoo.**
3. **Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu uliopita.**
4. **Kujadili yatokanayo na Mkutano Mkuu uliopita.**
5. **Kupokea na kujadili Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za mwaka 2019.**
   - **5.1** Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi.
   - **5.2** Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2019.
6. **Taarifa kuhusu Mtaji wa Benki.**
7. **Mabadiliko ya Katiba - AZIMIO MAALUM**
8. **Kuteua Wakaguzi wa Hesabu.**
9. **Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.**
10. **Kupanga mahali na tarehe ya Mkutano ujao.**
11. **Kufunga Mkutano.**

**MAELEZO:**

1. Daftari la Wanahisa litafungwa tarehe 11/09/2020 na litafunguliwa tena tarehe 14/09/2020.
2. Makabrasha ya Mkutano yatapatikana katika Makao Makuu ya Benki ya Wananchi Tandahimba tarehe 07/09/2020 na Ukumbini siku ya Mkutano.
3. Mwanahisa ana haki ya kumtuma mwakilishi kwa kujaza fomu maalum (proxy form).
4. Wanahisa au wawakilishi wao, watakao hudhuria Mkutano watajigharamia usafiri na malazi.

Kwa mawasiliano zaidi, tafadhali tumia anuani ifuatayo:

Katibu wa Benki,
TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC,
Kiwanja Na. 539 - Kitalu 'C', Barabara ya Namikupa,
S. L. P. 06, Tandahimba. MTWARA.

**KWA IDHINI YA BODI**

**J. B. Rugambo**
**Katibu wa Benki**

**TACOBA – BENKI yetu kwa MAENDELEO yetu**

**UKISIKIA TANGAZO HILI MJULISHE MWENZAKO**

215866102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hili la riba kubwa benki lipatiwe ufumbuzi sasa

**MALALAMIKO** ya wakopaji katika taasisi za fedha kuhusu riba kubwa husussan wananchi wa kawaida yameendelea kwa muda mrefu, licha ya mamlaka za serikali kuahidi kutafuta ufumbuzi.

Wakopaji wanalalamika kuwa viwango vikubwa vya riba vinawakwaza kukopa kwa kuwa wanapokopa mwanajikuta katika wakati ngumu unapofika muda wa kuanza kurejesha.

Pamoja na riba kubwa, taasisi rasmi za fedha zimekuwa zikitoa masharti magumu kwa wakopaji yakiwamo kuwa na mali zisizohamishika, ambazo Watanzania wengi wa kawaida hawana uwezo wa kuzimiliki. Kutokana na sababu hizo hususan masharti ya dhamana ya mikopo wananchi hao wakiwamo wajasiriamali wanaofanya shughuli mbalimbali za kujiingizia kipato wamekuwa wakitafuta njia za mkato kujipata mikopo hiyo kutoka kwenye taasisi zisizo rasmi, hivyo wakati mwingine kujikuta wakitozwa riba ambazo ni kubwa zaidi na haziendani na uhalisia.

Kutokana na hali hiyo, wapo waliojikuta wakilazimika kuuza mali zao na hata kufilisika ili kurejesha mikopo hiyo.

Kuna taasisi nyingi ambazo ziko nchini zikifanya shughuli za kukopesha fedha bila hata kusajiliwa, ambazo zimewapa wakati mgumu sana wananchi wengi wanaozikimbilia kukopa.

Hata hivyo, serikali imeshapitisha sheria ya kuzidhibiti ambayo ni Sheria ya Sekta Ndogo ya Fedha ambayo itaanza kutumika Novemba mwaka huu.

Mbali na kusubiriwa kwa utekelezaji wa sheria hiyo, serikali ilishaahidi mara kwa mara kuwa itahakikisha riba za mikopo katika sekta rasmi; kwa maana ya mabenki na taasisi zingine inashuka.

Umuhimu wa mabenki na taasisi za fedha kupunguza riba ya mikopo umekuwa ukielezwa kuanzia uongozi wa juu wa serikali ya awamu ya tatu na kuendelea hadi sasa, hoja kubwa inayoelezwa ikiwa ni kuwawezesha wananchi kukopeshwa na kuwapungumzia wananchi wa kipato cha chini mzigo na usumbufu wa kurejesha mikopo. Mawaziri na watendaji wakuu wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ni miongoni mwa viongozi wa serikali ambao kila uchao wanatoa maelekezo kwa benki na taasisi za fedha kuhakikisha kwamba riba zinapunguzwa ili kuwawezesha wananchi wengi kukopa na kushiriki katika shughuli za kupaisha uchumi wa nchi yetu.

Juzi Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alizitaka taasisi za fedha kuwa msaada kwa wananchi kwa kutoa riba nafuu zinazoweza kuwasaidia wananchi kiuchumi kuliko kutaka faida kubwa inayoweza kusababisha maumivu kwa wananchi wa hali ya chini. Akizungumza wakati wa uzinduzi wa benki ya NCBA jijini Dar es Salaam, Dk. Kijaji, alisema serikali haitavumilia taasisi za kifedha zenye malengo ya kuwakandamiza wananchi na kudidimiza uchumi wao na uchumi wa Taifa kwa ujumla.


Alisema tukisikia baadhi ya taasisi za kifedha zimekuwa na masharti yasiyokuwa rafiki kwa Watanzania wetu na benki zimekuwa na masharti magumu ya mikopo kwa wananchi wakiwamo vijana, kinamama pamoja na wakulima.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, juzi naye alirudia msisitizo huo kwa benki na taasisi za kushusha riba kwa wakopaji wakati wa kupokea gawio la serikali la Sh. bilioni 15.2 kutoka Benki ya NMB kwa mwaka jana jijini Dodoma kwamba mikopo inawatenga wenye kipato cha chini, hivyo aliwataka wenye benki kutafuta suluhisho. Sisi tunaona kuwa sasa kauli za kuzishauri taasisi za fedha kupunguza riba zimechukua muda mrefu bila wahusika kuchukua hatua za kutafuta suluhisho.

Hata hivyo, tunaamini kuwa kwa kuwa serikali ndiyo yenye kutunga sheria na sera pamoja na kuzisajili na kuzisimamia taasisi za fedha, ina uwezo wa kulazimisha agizo hilo kutekelezwa haraka iwezekanavyo.

Ni matarajio yetu kuwa taasisi hizo zitatii maelekezo hayo katika kuunga mkono juhudi za serikali za kupaisha uchumi kupitia uwezeshaji wa wananchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wananchi msiogope kuhoji ilani za vyama zitazonadiwa

Na Sabato Kasika

**OKTOBA** 28, mwaka huu, Watanzania watapiga kura kuchagua viongozi watakaowaongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo ikiwa ni wa sita tangu Tanzania iliporejesha siasa ya mfumo wa vyama vingi.

Kwa kawaida, katika uchaguzi wa kushindanisha vyama vingi vya siasa ili kutwaa dola na kuunda serikali, kila chama huandaa ilani yake ya uchaguzi, ambayo inayotafsiri na kuelezea sera za chama kuhusu maeneo muhimu ya siasa, uchumi na jamii.

Hutoa maelezo fasaha kuhusu mikakati ya utekelezaji wa sera zinazonadiwa ili wagombea wake wakifanikiwa kushinda watekeleze na hutoa ahadi kwa wananchi kuhusu mambo ambayo chama kitaelekeza na kusimamia serikali kuyatekeleza.

Kimsingi, ilani ya uchaguzi ni maelezo ya sera katika kipindi husika, na inalenga kuwaeleza wananchi ni mambo gani chama kitafanya iwapo kitashinda katika uchaguzi na kuunda serikali.

Hivyo, wakati huu ambao nchi inaelekea katika uchaguzi mkuu, ni nafasi pekee kwa Watanzania kupima ilani za vyama kwenye kampeni zinazotarajia kuanza wiki ijayo ili kujua kama zinafaa na zinatekelezeka.

Kipindi hiki cha kujenga uchumi wa kisasa na taifa linalojitegemea, ni muhimu kuwa na ilani ambazo zinatekelezeka, hivyo wananchi wasisite kuwahoji wagombea pale wanapoona kuna jambo hawalielewi katika ilani za vyama.

Ni muhimu kutambua kuwa uwezeshaji wananchi kiuchumi ni mikakati sahihi ya kujenga uchumi wa kisasa, hasa kwa kutambua hali na mazingira ya kisiasa, kiuchumi na kijamii katika karne hii.

Vilevile, jitihada zinapaswa kuchukuliwa ili kuboresha mazingira ya sasa ya kiuchumi na kisiasa, ili Watanzania wote waendelee kufaidi keki ya taifa lao kama ilivyoanza kuonekana baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015.

Binafsi ninaamini kwamba, wananchi wakiwa wepesi wa kuhoji ilani za vyama, mwisho wa siku watakuwa wamepata chaguo sahihi la kuwawezesha kufikia kile wanachokitaka kwa kuchagua viongozi sahihi.

Mvuto na ushawishi wa wagombea wa kutoka vyama mbalimbali vya siasa, usiwe kigezo bali wananchi wasikilize ilani waone kama zinalenga kuwasaidia kuinuka kiuchumi, pia waelewe ni jinsi gani zitatekelezwa.

Uzoefu unaonyesha kuwa, karibu vyama vyote huwa vina mwelekeo chanya wa kisera na vipaumbele katika maeneo kadhaa muhimu ikiwamo sekta ya uchumi huku vikitoa ahadi ya kuiboresha.

Kila chama kwa namna tofauti, kinaweza kuahidi kuiboresha kusimamia kwa kuweka sheria kali dhidi ya rushwa, ufisadi na kusimamia nidhamu kwa wafanyakazi wa sekta ya umma.

Yote hayo ni mazuri, lakini suala la msingi ni kuweka wazi jinsi ya kutekeleza ili wananchi waridhike na majibu hayo kuliko kukubali maneno matamu ya wanasiasa na kumbe ikiwa ni mbinu kutafuta kura.

Kwa sasa ila chama kina ilani yake ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025 ambayo itadadiwa kwenye kampeni ndiyo maana nikawataka wapigakura kwenda kusikiliza na kuhoji ili kupata wagombea sahihi.

Ikumbukwe kuwa, wanasiasa wana maneno matamu wawapo majukwaani, ambayo yanaweza kumfanya mwananchi akashawishika kuwapigia kura na kumbe hawana ni ya kweli ya kuleta maendeleo.

Hali hiyo inaweza kumalizwa na wananchi wenyewe kuwa wapesi wa kuhoji pale wanapoona kuna jambo ambalo halijakaa sawa au hawajaelewa lengo la ilani ya chama fulani wanachokishabikia.

Kuna dhana ya siasa ni uchumi, hivyo wananchi wajiandae kuchagua viongozi watakaowaboreshea maisha yao, na njia pekee ni kutoogopa kuhoji kile ambacho hakika sawa ndani ilani za vyama zitakazoanza kunadiwa wiki ijayo.

MWANGA HAKIKA

# TAARIFA KWA UMMA

Bodi ya Wakurugenzi ya "Mwanga Hakika Microfinance Bank Limited [MHB]" inapenda kuujulisha umma na wateja wake kuwa benki tatu zimeungana ambazo ni **EFC Tanzania Bank Ltd, Hakika Microfinance Bank Ltd** na **Mwanga Community Bank Ltd.**

Hivyo kuanzia tarehe 14 Agosti, 2020 benki hiyo itatumia jina la **"Mwanga Hakika Microfinance Bank Limited"** yenye matawi yake ambayo ni **Main Branch [Sky Tower -Kijitonyama, DAR], Tegeta [DAR], Arusha, Moshi, Mwanga, Same na Hedaru.**

***Kwa Maulizo , Tafadhali wasiliana nasi:***
**Mwanga Hakika Microfinance Bank Ltd**
**Barua pepe: info@mhbbank.co.tz;**
**Au tupigie : +255 22 276 0211/12**

## MATAWI YETU

**MAIN BRANCH - DSM**

MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK LTD,
SKY TOWER,PLOT No. 1 & 50,
Block No. 45A, KIJITONYAMA
NEW BAGAMOYO ROAD, P.O.BOX 11735,
DAR ES SALAAM –TANZANIA
Tel: +255 0788 408 508

**ARUSHA**

MWANGA HAKIKA MICROFINANCE LIMITED
PLOT NO 21,ARUSHA CONSULTANT HOUSE NO 12,
COL MIDDLETON ROAD, KALOLENI
ARUSHA - TANZANIA
TEL: +255 0755 059234

**MWANGA- KILIMANJARO**

MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK LIMITED
NEW MWANGA TOWN ,
FORMER NSSF BUILDING
MWANGA – TANZANIA
TEL: + 255 0752 635211

**HEDARU - KILIMANJARO**

MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK LIMITED
DAR- ARUSHA ROAD, NEW KIMWELI FILLING STATION
HEDARU- TANZANIA
Tel: +255 0754 233722

**MOSHI - KILIMANJARO**

MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK LIMITED
OLD MOSHI ROAD, FORMER NSSF BUILDING
MOSHI- TANZANIA
Tel: +255 0757 511 774

**SAME - KILIMANJARO**

MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK LIMITED
SAME TOWN, OPPOSITE POSTAL OFFICE
SAME - TANZANIA
Tel: +255 0744 811 766

**TEGETA- DSM**

MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK LIMITED
MJAPAN COMPLEX BUILDING
DAR ES SALAAM - TANZANIA
Tel: +255 0753 292158

215865702

HABARI KITAIFA

## Mgombea urais kufanya kampeni kwa baiskeli

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA urais kupitia Chama cha Demokrasia Makini, Cecilia Mwanga, amesema kampeni zitakapoanza, baadhi ya maeneo atakuwa anatumia baiskeli, pikipiki, guta na bajaji ili kuwafikia wananchi.

Jana, katika mahojiano maalum na Nipashe iliyotaka kujua kama chama chake kitafanya kampeni na kuifikia mikoa na wilaya zote za Tanzania, mgombea huyo alisema chama chake hakipati ruzuku, lakini kimejipanga kufanya kampeni nchi nzima na atatumia usafiri huo kuwafikia wananchi.

"Tutatumia usafiri wa baiskeli, bajaji, pikipiki na guta, siyo kwa sababu chama changu hakipati ruzuku, bali ni kutokana na baadhi ya maeneo miundombinu ni mibovu, hivyo magari hayawezi kufika," alisema.

Mwanga alisema maeneo mengi nchini kuna vikwazo vya kimiundombinu hususani vijijini ambako wananchi wana kiu kubwa ya kupata maendeleo, lakini bahati mbaya viongozi hawafiki huko kuwahamasisha.

Alisema kama wananchi watakipa ridhaa chama chake kushika dola, watahakikisha kinahamasisha lugha ya Kiswahili na kuzungumzwa katika nchi zote dunia.

Alisema pamoja na kwamba lugha ya Kiswahili inazidi kukua, bado nchi nyingi dunia hazizungumzi lugha hiyo.

"Tukiingia madarakani tutahakikisha lugha ya Kiswahili inakuwa lugha ya mawasiliano ya kibiashara kwa nchi zote, hilo linawezekana kwani tuna wataalamu wengi," alisema.

Alisema mambo mengine atakayoyafanya ni kuhamasisha kilimo, afya na elimu kwa sababu sekta hizi zinagusa sana maisha ya wananchi wa chini.

# Kabudi: Mradi wa reli ya TAZARA hautakufa

**Na Halfani Chusi**

TANZANIA imeihakikishia Serikali ya China kuwa mradi wa reli ya Tanzania-Zambia (TAZARA) uliojengwa kwa msaada kutoka Serikali ya China hautokufa kutokana na mradi huo kuwa na manufaa makubwa.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba Kabudi, alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya uzinduzi wa kitabu cha Kumbukizi ya Urafika Kati ya China na Afrika.

Profesa Kabudi alisema Serikali ya China imekuwa na uhusiano mzuri na Tanzania kwa kipindi kirefu, akibainisha kuwa hata wakati Wachina wanatoa msaada wa kujenga reli hiyo, nchi yao ilikuwa maskini.

"Serikali ya China kwa kushirikiana na Rais wa Awamu ya Kwanza wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, walikuja kutupa msaada wa kujenga reli wakati hali yao ilikuwa mbaya kiuchumi, walikuwa maskini, lakini bado waliona kuna umuhimu wa Tanzania kupata reli itakayosaidia nchi nyingine ambazo zitanufaika na reli hiyo kama Zambia na nyinginezo," alisema.

Profesa Kabudi aliongeza: "Serikali ya China imekuwa ikitupiga tafu katika sekta nyingi ikiwamo kilimo, jeshi, viwanda. "Kwa hiyo, niwatoe hofu Serikali ya China kuwa Serikali ya Tanzania ipo bega kwa bega na inatambua mchango wenu."

Waziri huyo alisema serikali ilitoa Sh. bilioni 10 kwa ajili ya maboresho ya reli hiyo na kulipa mishahara kwa baadhi ya wafanyakazi wa reli hiyo.

"Baada ya serikali kutambua kuwa mradi huo una manufaa makubwa, tulitoa kiasi cha Sh. bilioni 10 kwa ajili ya kulipa wafanyakazi mishahara pamoja na maboresho kadhaa ambayo kimsingi yalihitaji pesa na tutaendelea kusaidia kwa kuwa hii ni reli yetu wenyewe na inatusaidia sisi wenyewe," alisema.

Msaidizi Mkuu wa Meneja Mkuu wa TAZARA, Jofrey Sengo, alisema Sh. bilioni 10 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya maboresho ya reli hiyo zimesaidia pia kuongeza morali ya watumishi wao.

"Serikali baada ya kutupatia hizo pesa tulizigawanya katika makundi mbalimbali, zingine ziliingia katika kulipa mishahara ya wafanyakazi, kununua mitambo ambayo inatusaidia kupasua kokoto katika kiwanda cha kokoto kilichoko Mbeya pamoja na vipuli vya injini," alisema.

Katika hafla hiyo, Balozi wa China nchini, Wang Ke, aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa kuendelea kushirikiana na China, akisisitiza kuwa uhusiano kati ya nchi hizo mbili ni mzuri.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa miundombinu ya barabara za juu (Ubungo Interchange), katika makutano ya Barabara ya Sam Nujoma, eneo la Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: REBECCA MWIHOMEKE/TUDARCO**


Ujamaa Community Resource Team
EMPOWERMENT JUSTICE STEWARDSHIP

215866202

PO Box 15111, Arusha, Tanzania
www.ujamaa-crt.org

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI.**

SHIRIKA LA UJAMAA COMMUNITY RESOURCE TEAM NI SHIRIKA LISILO LA KISERIKALI LINALOJISHUGHULISHA NA KUJENGA UWEZO WA JAMII KATIKA MASUALA YA UTAWALA BORA, ARDHI NA MAZINGIRA KATIKA MIKOA YA ARUSHA NA MANYARA.

SHIRIKA LINAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA LITATEKELEZA MIRADI MIPYA IPATAYO MIWILI KAMA INAVYOAINISHWA HAPA CHINI KUANZIA AUGUST 2020 MPAKA 2021

1. UCRT KWA UFADHILI KUTOKA THE NATURE CONCERVANCY TUTATEKELEZA MRADI WA ``USIMAMIZI JUMUISHI WA NYANDA ZA MALISHO`` UTAKAOGHARIMU KIASI CHA SHILINGI 20,890,877 KATIKA VIJIJI VYA KITWAI B, MBAASHI NA SUKURO KATIKA WILAYA YA SIMANJIRO.
2. UCRT KWA UFADHILI KUTOKA MALIASILI INITIATIVES TUTATEKELEZA MRADI WA KUWAJENGEA WANAWAKE UWEZO KIUCHUMI UTAKAOGHARIMU KIASI CHA DOLA 160,000 KATIKA WILAYA NNE AMBAZO NI MONDULI, SIMANJIRO, NGORONGORO NA KITETO.

***MIRADI HII YOTE ITATEKELEZWA KWA KUSHIRIKIANA NA HALMASHAURI HUSIKA PAMOJA NA VIJIJI.***

KWA MAWASILIANO ZAIDI director@ujamaa.or.tz na manager@ujamaa-crt.or.tz


# Kampuni zatakiwa kutenganisha taka

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), imezitaka kampuni za ukusanyaji taka kuzingatia kutenganisha taka za kawaida na zenye kemikali ili kuepusha madhara kwa jamii.

Rai hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Ofisa Ukaguzi wa GCLA, Emmanuel Lewanga, katika mafunzo ya siku moja kwa maofisa biashara 39 wa Wilaya ya Ilala, yaliyotolewa na Ofisi ya Kanda ya Mashariki.

Alisema kampuni zinazozoa taka zimekuwa zikichanganya taka hizo, hivyo wakati wa kuziteketeza huleta madhara kwa jamii inayozunguka eneo zinakoteketezewa.

"Niombe kila manispaa kutoa elimu kwa kampuni mlizozisajili kuzoa taka, wazitenganishe wakati wa kuzikusanya na kabla ya kuziteketeza kwa sababu uteketezaji wa taka zenye kamikali na za kawaida ni tofauti," alisema Kewanga.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala, Jumanne Shauri, akifunga mafunzo hayo, aliishukuru GCLA kwa kuyaandaa, kwa sababu yatawasaidia katika kuwatambua na kuwasajili wafanyabiashara wanaojihusisha na kemikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Kanda ya Mashariki. "Nimefarijika kwa mafunzo kutoka GCLA, naamini yatawaongezea weledi maofisa biashara katika majukumu yao ya utoaji leseni kwa wafanyabiashara wanaojihusisha na biashara za kemikali. Itasaidia kutoruhusu watu wafanye biashara ya kemikali bila kuwa na vibali na kusajiliwa na m amlaka," alisema Shauri.

Alisema watahakikisha maofisa hao wanashirikiana na mamlaka, katika kuhakikisha wanapata barua za utambulisho au usajili kabla ya kupewa leseni ya biashara.

Shauri aliendelea kusema kuwa, watashiriki katika kufanya ukaguzi wa kutambua wafanyabiashara ambao walipewa leseni za biashara na wanajihusisha na biashara ya kemikali bila kutambuliwa na mamlaka kwa lengo la kusaidia wasajiliwe ili kulinda afya za wananchi na mazingira kwa sababu kemikali ni hatari zisiposimamiwa kikamilifu.

"Itabidi kufanya ukaguzi wa maduka yanayouza kemikali ili kuweza kutambua kama wamesajili lengo ni kuwalinda walaji, tutashirikiana kutambua kemikali zinazouzwa hazina madhara kwa watumiaji na wahusika wamesajiliwa ili kulinda afya zetu na mazingira" alisema Shauri.

HABARI KITAIFA

# NHIF yaongeza dawa 71 katika kitita

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) imeboresha orodha ya dawa muhimu kwa kuongeza aina 71 ambazo hazikuwapo awali katika orodha husika na kusababisha malalamiko kutoka kwa wananchi.

Kupitia maboresho hayo, NHIF imeongeza dawa hizo katika kitita chake cha mafao kitolewacho kwa wanufaika wake kuanza kutumika mara moja nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa, Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, alisema lengo lake ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya wananchi wanazipata mpaka ngazi ya halmashauri na kufika katika kijiji. "Serikali imeongeza aina ya dawa 71 ambazo hazikuwapo awali katika orodha husika na kusababisha malalamiko kwa wananchi, kuhanisha maeneo ya ushirikiano baina ya NHIF na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ili ziweze kuleta tija kwa wananchi," alisema.

Prof. Makubi alisema kuwa mikakati hiyo imekwenda sambamba na serikali hivi sasa kuongeza bajeti ya dawa kutoka shilingi bilioni 30 mwaka 2015 hadi kufika shilingi bilioni 270, kuboresha miundombinu ya huduma za hospitali ukiwamo ujenzi wa zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya na za rufani za mikoa.

Alisema kuwa kwa kutambua umuhimu wa bima ya afya kwa wananchi na huduma zitolewazo MSD, serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imekutanisha na viongozi waandamizi wa NHIF pamoja MSD kwa lengo la kupanga mikakati ya utatuzi wa changamoto mbalimbali zitakazojitokeza katika utekelezaji wa majukumu hayo mapya.

Kwa upande wa Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, alisema kuwa wamejipanga kuhakikisha utekelezaji wa makubaliano hayo yaliyofanyika kati yao na MSD ya kutoa huduma bora kwa kuongeza orodha ya dawa inapatikana kwa wakati na maeneo yote yanafikiwa hasa ngazi ya vijijini kwenye zahanati.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Brigedia Jenerali Dk. Gabriel Mhidize, alisema kuwa kwa kupitia uzoefu waliupata katika usambazaji wa dawa katika Wilaya ya Chato mkoani Geita, Wilaya ya Mbeya na Dar es Salaam wanaamini watasambaza dawa hizo nchini katika hospitali zote za wilaya ili ziweze kupatikana kwa bei nafuu.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitano inayokwisha, serikali imeweza kuboresha huduma za upatikanaji wa dawa na vifaa tiba nchini na kuokoa fedha zake kiasi cha shilingi bilioni 760 ambazo zilikuwa zikitolewa kwa ajili ya kugharamia matibabu ya wagonjwa nje ya nchi.

Dk. Mollel alisema kuwa kutokana na maboresho hayo, huduma hizo zilizokuwa zikilazimika kufanywa nje hivi sasa zinafanyika nchini, na kwamba zaidi ya nchi 16 zinakuja kupata huduma hizo nchini kutokana na kuwapo kwa kiwango cha chini ukilinganisha na nchi nyingine.

# Mpina akipigia debe kiwanda

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Kilimo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amesema kuna haja kubwa ya kukisaidia kiwanda cha Meat King Fish Distributor ili kiendelee kuchakata kwa nguvu zote nyama ya ng'ombe, mbuzi na kondoo na mazao mengine ya mifugo.

Akizungumza jijini Arusha, Mpina alisema kufanya hivyo kunaboresha maisha ya wakulima, wafugaji na wavuvi.

Akizungumza baada ya kutembelea kiwanda hicho akifuatana na Kaimu Mkurugenzi wa Mikopo wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Jeremiah Mhada, Waziri Mpina ameitaka kuendelea kuvisaidia viwanda vinavyowasaidia wazalishaji mali wengi hapa nchini.

TADB imekuwa ikifanya kazi kubwa katika kuwasaidia wakulima, wavuvi na wafugaji wa nchi hii. Jitihada hizo ziendelezwe ili wadau wa sekta hizo wazidi kunufaika uboreshwaji wa mnyororo ya thamani katika sekta zao, amesema Waziri Mpina. Alisema kuwa kuimarika kwa uzalishaji wa kiwanda hicho kunaleta manufaa kwa Watanzania kwani kunapunguza ukosefu wa ajira kwa Watanzania na kunaimarisha ajira za wafugaji na kuwafanya wawe na uhakika wa soko la bidhaa zao.

"Uimarishwaji wa uzalishaji katika kiwanda hiki utasaidia kutengeneza ajira mpya na kuimarisha ajira za zamani kwa wadau wa kilimo, ufugaji na uvuvi,'' alisema na kuongeza kuwa uchumi wa viwanda hautakuwa na maana kama sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi hazitafanyiwa mageuzi makubwa.



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji (katikati), akipokea zawadi kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya benki mpya ya NCBA aliyemaliza muda wake, Sharmapal Aggarwal, baada ya kuizindua rasmi benki hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Ofisa Mkuu Mtendaji wa Benki hiyo, Margaret Karume. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Baba jela miaka 30, kucharazwa bakora 12 kwa kubaka mwanawe

**Na Said Hamdani, LINDI**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Lindi, imemuhukumu mkazi wa Kijiji cha Mahiwa, Kata ya Nyangao, Maulidi Salum (25), kifungo cha miaka 30 jela, kuchapwa viboko 12 na kumlipa mlalamikaji fidia ya Sh. milioni 2 baada ya kupatikana na makosa mawili, likiwamo la kumpa ujauzito mwanawe wa kufikia ambaye ni mwanafunzi.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi, Maria Batraine, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka na mwenyewe kukiri makosa yake.

Hakimu Batraine akitoa hukumu kupitia Sheria ya Elimu kifungu cha 60 A fungu dogo la (3) Sheria ya Elimu alimhukumu kosa la pili la kumpa mimba na kukatisha masomo ya mwanafunzi huyo kifungo cha miaka 30 jela pamoja na kuchapwa viboko 12, na atakapomaliza kutumikia adhabu yake amlipe mlalamikaji fidia ya Sh. milioni 2.

Awali, Mwanasheria wa Serikali, Godfrey Mraakitoa, aliiambia Mahakama hiyo kwamba siku isiyofahamika Machi mwaka huu, mshtakiwa akiwa ni baba wa kufikia wa mkewe, alimbaka mtoto huyo (jina limehifadhiwa) mwenye umri wa miaka 13, ambaye anasoma Shule ya Msingi Mahiwa na kumpa ujauzito.

# Umuonapo mtoto huyu toa taarifa

**Na Mary Geofrey**



MTOTO Beatha Mwesiga (14) (pichani), anatafutwa na wazazi wake baada ya kutoweka nyumbani kwao mtaa wa Kitunda Machimbo, wilayani Ilala jijini Dar es Salaam.

Mtoto huyo alitoweka Agosti 11, mwaka huu majira ya saa 5:00 asubuhi, wakati alipokuwa akiosha vyombo nje ya nyumba wanayoishi.

Shangazi wa Beatha, Justamary Matunda, alilieleza Nipashe kuwa, mtoto huyo alikuwa nyumbani akiosha vyombo nje ya nyumba kabla ya kuondoka.

"Walikuwa wanakunywa chai asubuhi alipomaliza muda kama saa 4:00 akapewa maelekezo ya kuosha vyombo nje ya nyumba tunayoishi, mdogo wangu akiwa ndani anajiandaa kwenda kwenye shughuli zake ndipo alipotoka na kumkosa," alisimulia Matunda.

Alisema mtoto huyo ni wa binamu yake na alikuja Dar es Salaam wiki mbili zilizopita akitokea Kijiji cha Kangantebe karibu na Hospitali ya Bugando wilayani Muleba mkoani Kagera kwa ajili ya kuja kujifunza kushona nguo.

Alisema binti huyo alimaliza darasa la saba mwaka jana, lakini hakufaulu ndipo mama yake mzazi alimuomba amchukue kuja Dar es Salaam kwa ajili ya kujifunza kushona.

Matunda alisema siku chache baada ya kukaa naye alianza kulalamika kutaka kurejea nyumbani kwao Muleba kwa sababu hajazoea mazingira kwa sababu tangu alipofika alikuwa akiugua malaria.

"Kabla ya kutoroka aliahidi watu ninaioshi nao ndani kuwa atatoroka hata kwa miguu kurudi kwao. Lakini siku ya tukio hakuwa amegombana na yeyote," alisema Matunda.

Alisema wamemtafuta bila mafanikio yoyote na waliripoti kituo cha Polisi Kitunda na kutoa taarifa na kupewa hati yenye namba KIT/RB/2684/20, Taarifa 12/08/20.

Aliwaomba watakaomuona watoe taarifa katika kituo cha polisi kilicho jirani au kupiga simu namba 0788262786 au 0713262785 na 0767262787.

## Wakazi zaidi Shinyanga kunufaishwa maji ya Ziwa Victoria

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

Wananchi wa Kata ya Mwakitolyo Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wanatarajia kuondokana na adha ya kutumia maji yasiyo salama kiafya, baada ya mradi mkubwa wa maji toka Ziwa Victoria kuanza kutekelezwa chini ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama na Shinyanga (KASHWASA).

Mkurugenzi wa mamlaka hiyo, Mhandisi Joshua Mgeyekwa, alisema juzi kuwa mradi huo kwa sasa upo katika hatua ya ulazaji wa mabomba ambayo yatapeleka maji kwenye tanki kubwa lilioko Mwakitolyo kutoka Solwa ili kuwezesha utoaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi.

Alisema mradi huo wa maji ya Ziwa Victoria umefanyiwa usanifu upya kwa ushirikiano wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), pamoja na Kashwasa, baada ya hapo awali kusimamiwa na halmashauri husika, na kushindwa kutoa huduma ya maji kwenye kata hiyo.

"Baada ya kufanya usanifu upya, tumebadilisha aina ya mabomba na kuyatoa ya awali ambayo yalikuwa ya plastiki na kuweka mabomba ya chuma, yenye uwezo wa kuimili msukumo mkubwa wa maji (presha ya maji), inyaofikia zaidi ya mita 400 PN 40, ambapo maji haya tunayachukulia Solwa na kuyaleta Mwakitolyo," alisema Mugeyekwa.

"Mpaka sasa hivi ujenzi umefikia asilimia 60 na tulitegemea tujenge mradi huu kwa siku 90 yaani miezi mitatu, lakini sasa hivi tumetumia siku 45, lakini ndani ya mwezi mmoja au zaidi tutakuwa tumemaliza na mradi huu una gharama ya shilingi bilioni 2,3," aliongeza.

Kwa upande wake mkuu wa wilaya ya Shinyanga Jasinta Mboneko, aliutaka mradi huo wa maji utekelezwe haraka kabla ya mvua kuanza kunyesha, ili wananchi wa Kata hiyo ya Mwakitolyo waanze kutumia maji hayo kutoka Ziwa Victoria, na kuondokana na adha ya matumizi ya maji ambayo siyo salama.

"Mahitaji makubwa ya wananchi wa Kata ya Mwakitolyo ni kupata majisafi na salama hicho ndicho kilio chao kikubwa, na mimi nimefanya ziara kuja kujionea hatua ya utekelezaji wa mradi huu wa maji kutoka Ziwa Victoria, naomba mradi huu ukamilike haraka kabla msimu wa mvua haujaanza," alisema Mboneko.

Pia, aliwataka wananchi hao kuitunza miundombinu hiyo ya maji na kutoiharibu, ili idumu kwa muda mrefu na kutoa huduma ya majisafi na salama, na kuondokana na changamoto mbalimbali zilizokuwa zikisababishwa na ukosefu wa majisafi kwenye kata hiyo.

# Madereva walia uchafu vyoo vya Manispaa

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MADEREVA wa usafirishaji abiria waendao vijijini mkoani Kagera, wameiomba Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba kutafuta ufumbuzi wa usafi wa vyoo vilivyojengwa kwa ajili ya watumiaji wa stendi ya muda.

Madereva hao walihamishwa kutoka stendi kuu ya mabasi na magari madogo mkoani hapa na kupatiwa stendi ndogo ya muda iliyopo Mtaa wa Jamhuri Kata ya Miembeni ili kuondoa msongamano uliokuwa ukikatazwa wakati wa ugonjwa wa COVID-19. Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti Hemed Juma, Enock Mwemezi na Athman Byonabusha walieleza manispaa ndiyo yenye kuangalia taratibu za afya za walipaushuru wao.

Mwemezi, dereva wa gari liendalo Kata ya Izibya, alisema hali ya uchafu wa vyoo ikiendelea hivyo, kuna uwezekano wa kuwa na mlipuko wa magonjwa kwani hakuna huduma za usafi haziridhishi licha ya kukusanywa mapato kabla ya kuingia chooni

"Kuna hatari ya mlipuko wa ugonjwa hapa kwani hakuna usafi, vyoo vyetu vimejaa maji kwani vimejengwa kwa muda wakati wa corona, lakini hadi sasa hatuna pa kwenda, na gharama ya huduma chooni ni shilingi 300, wanakusanya manispaa," alisema Mwemezi.

Alisema katika stendi hiyo kuna matundu mawili pekee ya jinsi ya kike na kiume, lakini wanaume hujisaidia haja ndogo nje ya tundu kwa kushindwa kuingia ndani ikilinganishwa na idadi kubwa ya abiria na madereva.

Athuman Byonabusha, dereva wa gari dogo liendalo Kata ya Maruku, alisema stendi hiyo ilielezwa kuwa itakuwa ya muda, lakini imekuwa ya kudumu, madereva na abiria waangaliwe suala la usafi wa mazingira ya choo kwa kuwa gharama zinalipwa," alisema. Iweje wao manispaa wasiweke mazingira ya afya kwa kuwa ndiyo kila kitu," alisema na kuongeza:

"Leo ukitokea mlipuko wa ugomjwa wa kipindupindu itaonekana hakuna wanachokifanya," nikitoka stendi nalipa shilingi 1,000 nikienda choo nalipa 300 iweje washindwe kuweka usafi wa mradi wao."

Katibu wa Chama cha Madereva mkoani Kagera, Hemed Juma, alisema lengo la kufanya mgawanyiko huo ni kuondoa msongamo stendi kuu ya mkoa ambayo ina kila huduma rafiki inayotakiwa na madereva walipo stendi ya pili.

Aidha, alisema suala hilo limepelekwa kwa uongozi wa manispaa kwani ndiyo wenye jukumu la usimamizi wa mapato yanayotozwa katika stendi hiyo kama sehemu ya vyanzo vyao.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Moris Limbe, alisema uongozi unafanya maboresho katika vyoo kila mwezi kwa kutapisha kuondoa uchafu na maji yanayojaa.

Alisema muundo wa matundu hayo yana kina kidogo ndiyo sababu maji hupanda juu, hivyo watumiaji yanawapa shida katika utumiaji.

Hata hivyo alisema matarajio yalikuwa kuwarudisha stendi ambayo walikuwa wakitumia awali, lakini bado wanaangalia hali ya ugonjwa wa corona ili kuona kama itawezekana kuwarudisha eneo la zamani.




Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, akishuka kwenye meli mpya ya MV Butiama, baada ya kuwasili wilayani Ukerewe juzi. Meli hiyo, ilitambulishwa rasmi na kuanza kutoa huduma kwa abiria. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# TPSF yapongeza ununuzi ndege ya mizigo

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imepongeza serikali kwa kununua ndege ya mizigo, na kusema hatua hiyo itasaidia sana kuimarisha sekta ndogo ya kilimo cha matunda na mboga.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mkutano wa sekta binafsi na sekta ya umma, Mwenyekiti wa Bodi ya TPSF, Bangelina Ngalula, alisema ndege ya mizigo itasaidia kukuza biashara ya mboga na matunda na kuchochea uzalishaji katika sekta ndogo hiyo.

"Sekta ya mboga na matunda imekuwa ikikabiliwa na changamoto nyingi, hususani namna ya usafirishaji na uhifadhi wake. Bidhaa hizi zinahitaji miundombinu maalum ya kupoza mazao (cold rooms) ili yakea muda mrefu pasipo kuharibika," alisema Ngalula, na kueleza kwamba wafanyabiashara wa bidhaa za mboga na matunda wamekuwa wakipata shida ya kusafirisha bidhaa zao kwenye masoko ya nje kwa kuwa hazipo ndege za mizigo.

"Sekta hii inahitaji isimamiwe kwa makini kwani ina mchango mkubwa sana katika pato la Taifa, inaingiza fedha za kigeni. Ni muhimu serikali kuendelea kuboresha mazingira ya biashara ili sekta hii iweze kufanya kazi kwa ufanisi," alisema Ngalula, na kueleza kwamba wakulima katika sekta ndogo hii ni watu wenye kujituma sana, wanaingiza fedha ya kigeni na kukuza ajira, jambo ambalo amesema halifahamiki kwa watu wengi.

Alitoa rai kuwa katika vikao vijavyo wahudhurie wawakilishi wa Polisi Usalama Barabarani , Wakala wa Barabara (TANROADS) na Mamlaka ya Uthibiti wa Usafiri Ardhini(LATRA) ili wajenge uelewa juu ya bidhaa hizo ambazo ni rahisi kuharibika, na wazipe kipaumbele katika maeneo yote ili zisafirishwe kwa haraka.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chama cha Wakulima wa Mboga na Matunda (TAHA), Dk. Jacqueline Mkindi, alisema ndege ya mizigo itakua ni chachu ya uzalishaji mboga na matunda na kueleza kwamba ni muhimu kuimarisha usimamizi wa sekta ndogo hiyo kuanzia shambani mpaka sokoni.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, aliyekuwa mwenyekiti wa kikao hicho, alisema serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini, na kuongeza kwamba ununuzi wa ndege ya mizigo ni moja kati ya hatua zinazochukuliwa kurahisisha usafirishaji wa bidhaa za mboga, matunda, nyama na minofu ya samaki.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Waziri Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina; Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe; Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango; Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa; Naibu Waziri Kilimo, Hussein Bashe na Makatibu Wakuu wa Wizara hizo.




Ukurasa 13

## Utitiri wa vyama dhaifu hauna afya katika siasa

BUFE
IJUMAA AGOSTI 21, 2020
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 12

## EWURA: Biashara ya madumu ilifanya petroli itoweke vituoni, tunapambana

JANGA LA RUFIJI...

# Tembo watatu wafunga mashine kusaga na 'kuvuna' mahindi ya wakulima 100

• Mmiliki ahamia vibarua; wahusudu maembe, sumu yao pilipili

**Na Beatrice Shayo, Rufiji**

MUSSA Hassan, mfanyabiashara mwenye umri wa miaka 35, mkazi wa kijiji cha Mloka Rufiji, ana simulizi ya majonzi, jinsi tembo wanavyomtesa katika mashine yake ya kusaga na kutamani kukimbia ajira ya vibarua.

Hassan, mwenye watoto watatu anasema kipindi cha nyuma alikuwa anapata mapato kati ya Sh. 20,000 hadi 30,000, pale alivyoanza kuvamiwa na tembo amejikuta akiambulia mapato Sh 3,000 kwa siku na hata kuikosa.

Anasema amejikuta akitumia muda mwingine kutengeneza mashine badala ya kufanya shughuli zake za kusaga, huku tembo wameongezeka ikilinganishwa na zamani.

"Hasara kubwa ni kwenye hili banda na chombo cha kukobolea wanapofika wanakula pumba pamoja na kuharibu hii mashine. Kama mwaka jana alibomoa hili banda lote nikajenga tena upya," anasema Hassan.

Baada ya kutengeneza banda hilo, anasema tembo hao watatu, iwaliendelea kumfanyia uharibifu kwa zaidi ya mara 12 na imemlazimu kutoa taarifa kwa serikali ya kijiji.

Anasema tembo hao wapo watatu na mara nyingi lazima wafike katika banda hilo, hivyo amejikuta akipoteza muda mwingi katika kulitengeneza badala ya kusaga mahindi.

"Hawa tembo wameniathiri kwa kiasi kikubwa, mara ya mwisho nimeenda ofisi ya kijiji nikakutana na Ofisa Mtendaji nikamuambia hii kazi naona inanishinda maana natumia gharama nyingi bora mtendaji kanifanyia mpango niende Stiegler's Gorge(mradi wa umeme) kufanya kibarua.

"Mtendaji aliniahidi kunifanyia huo mkakati..kwanza akanishauri unaonaje kama ungehama hilo eneo, nikamuambia kujenga kituo kingine ni gharama kubwa ni afadhali niachane na hii biashara niende kufanya kibarua,"



Mwenyekiti wa Kijiji cha Mloka, Rufiji, Chake Mkali. **PICHA ZOTE: BEATRICE SHAYO.**

Mfanyabiashara Mussa Hassan, akiwa ndani ya mashine ya kusaga nafaka kijijini Mloka, Rufiji, anayelalamika imeshaharibiwa na tembo zaidi ya mara 12 na wateja wamekimbia.

**VIONGOZI VIJIJI**

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mkange, Ally Didunda, anakiri uvamizi wa tembo shambani kwake, akisema: "Nimelima mahindi ekari tatu, wamenisafisha nimevuna eka moja na wakwe zangu walilima eka mbili akaambulia eka moja."

Anasema, alitegemea mapato ya Sh. milioni 1.5 kwa ajili ya kulipa ada ya mtoto wake anayesoma chuo kikuu, hajafanikiwa.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mloka, Ali Mbiteheni, anasema wamepakana na Pori la Akiba la Selous, hivyo wanyama wengi hufika kwenye makazi yao hasa tembo na wanafanya uharibifu kwenye mashamba na rasilimali zingine.

Anasema, kati ya Aprili na Mei mwaka huu, jumla ya wananchi 50 wa kijiji walivamiwa mashambani na mazao kuliwa na tembo na taarifa walishazipeleka wilayani na kwa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa).

Mbiteheni anasema, kuna wakati wanatoa taarifa za uvamizi na kwa wahusika na wanajibiwa 'tupo kwenye majukumu mengine' hali inayowaacha njia panda.

**UJANGILI?**

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mloka, Chake Mkali, anasema kwa kiasi ujangili ulikuwa juu, umemalizika kwani awali walikuwa wakisifika kwa vitendo vya biashara haramu ya ujangili kutokana na elimu iliyotolewa kupambana na ujangili nao.

"Hapa Mloka kwa sasa watu wanaogopa ujangili, zamani ni vigumu kuona tembo katika makazi yetu au kuharibu mazao. Kwa sasa tunaweza kusema tembo wameongezeka kila siku lazima tuwaone na tunapokea malalamiko ya kuharibu mazao ya wananchi," anasema

Mkali anasema awali wenyeji walitumika kuwapokea na kuwahifadhi majangili, lakini baada ya kuona serikali inawafuatilia, wameacha.

Anasema waliazisha mdadala wa kufuga nyuki na vikoba na waliojihusisha na uvuvi haramu, sasa wakazi 300 wameajiriwa kwenye miradi ya ujenzi wa umeme tangu mwaka jana.

Ombi la Mwenyekiti Mkali ni kwamba, serikali iwapatie askari wanyamapori kijijini, kuisaidia kudhibiti tembo ili wanaoingia kijijini na kufanya uharibifu.

"Wakulima wamekimbia mashamba yao, baada ya mazao yao kuliwa na tembo. Sasa wataendelea kukaa ili wafanyaje inabidi wahame na hapa tunategemea kilimo cha mahindi, mpunga na ufuta," anasema, huku akitaka hofu ya wakazi kukumbwa na njaa mwaka huu.

**KINGA YA PILIPILI**

Mhifadhi Wanyamapori Wilaya ya Rufiji, Mwarabu Mpunde, anataja mbinu ya ku-

ENDELEA UK.14

BIASHARA

# EWURA: Biashara ya madumu ilifanya petroli itoweke vituoni, tunapambana

- Yashuhudia maeneo kuuzwa lita Sh. 7000
- Uchaguzi mahitaji yapo juu, yatapatikana

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

BIDHAA ya mafuta ya petrol, umuhimu wake unajulikana kila mahali duniani. Kuna wafanyabiashara wasio waaminifu wamekuwa wakitumia njia mbalimbali kurudisha nyuma jitihada za upatikanaji, kwa manufaa yao binafsi.

Hivi karibuni, kulitokea changamoto ya upatikanaji bidhaa hiyo nchini, kukitajwa sababu wamiliki wa vituo vya mafuta na ufichaji bidhaa hiyo, kusubiri iadimike na wao wauze kwa bei ya juu.

Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Titus Kaguo, anasema upatikanaji mafuta ndio usalama wa Taifa, lakini kumekuwapo hujuma za wafanyabiashara na wasio waaminifu wanachangia bidhaa hiyo kuadimika.

"EWURA tunaendelea kuchukua hatua, ikiwamo kuwafungia vituo na kuwafutia leseni kwa mujibu wa sheria zilizowekwa," anatamka na kuendelea:

"Hao wanaoficha wanauza kwa kutumia madumu na wanauza kwa bei ya juu, ili wao wapate faida na kuwatesa Watanzania wenzao.

"Sasa hatua ambazo EWURA inazichukua ni kuwafungia au kuwafutia leseni kwa mujibu wa sheria....imechunguza na kubaini kuna baadhi ya vituo vimekuwa vikikiuka sheria vinatoa mafuta kwenye visima na kuweka kwenye madumu.

"Tumeshalijua suala hilo na wiki mbili zilizopita kuna mtu alinunua mafuta kule Ifakara lita moja kwa sh. 7,000, kule Mbinga wanauza kwenye madumu, hivyo tutahakikisha tunawakamata wote wanaofanya hivyo na adhabu ni kubwa."

Anatadharisha kuwapo njama za namna hiyo, huku katika zama iliyopo kuna kampeni bidhaa hiyo imekuwa ikiuzwa kwa bei kubwa zaidi na inatumika kwa kiwango cha juu.

"Tutawasaka wote kwa kutumia jeshi la polisi, ili kudhibiti hali hiyo na mafuta yawepo ya kutosha, kwa mfano baadhi ya vituo ikiwemo Mbinga (mkoa Ruvuma), wamiliki wengi wamekuwa wakifanya mchezo huu, jambo ambalo linasababisha bidhaa hiyo kutopatikana," anakaripia.



Waendesha pikipiki wilayani Mbinga, wakiwa katika foleni ya kununua mafuta katika kituo kilichopo mjini hapa. Wilaya hiyo inatajwa kuwa sehemu mojawapo ambako mafuta yalitoweka kwa kufichwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**UAGIZAJI WAONGEZWA**

Anasema mwezi Juni, matumizi ya mafuta yalipanda kwa asilimia saba huku Julai yakipanda kwa asilimia 12, akiyatolea ufafanuzi kwamba: "Hawa waagizaji wanaagiza mafuta kwa miezi miwili ya nyuma.

"Kwa mfano, mafuta ambayo matumizi yake yamepanda kwa mwezi Julai, ni mafuta yaliyoagizwa mwezi wa Aprili, ambayo yalikuwa yameshuka kwa asilimia saba na shughuli nyingi zilisimama kwa sababu ya Corona."

Anasema mfumuko wa biashara ulienda tofauti na mipango ambayo wafanyabiashara walipanga ya uagizaji wa mafuta.

Kaguo anasema ili kujitosheleza kwa mahitaji ya mafuta nchini kuanzia mwezi ujao, EWURA imeongeza makadirio ya matumizi kwa siku kuwa lita milioni 4.812 kwa petroli na lita milioni 6.082 kwa dizeli, hivyo Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa pamoja (PBPA), itatumia makadirio hayo kuagiza mafuta.

Anasema wameshaiagiza PBPA kuhakikisha inaingiza meli mbili za mafuta hayo mwezi huu, kwa sababu nchi inaelekea kwenye kipindi cha uchaguzi mkuu na mafuta ni bidhaa muhimu sana kukidhi mahitaji hayo yanayotumika kwa kiwango kikubwa.

Kaguo anasema, mafuta yanapatikana na inapotolea kundi au eneo filani wanakosa mafuta, ni vyema wakatoa taarifa kwa EWURA ili wasaidiwe huduma hiyo ipatikane kirahisi na kwa haraka.

Mwishoni mwa Julai mwaka huu, EWURA ilisema meli yenye lita milioni 67 za mafuta ingeingia nchini mwezi huu, ili kuhakikisha yanakuwepo mafuta ya kutosha, hususani pindi kampeni za uchaguzi zitkapoanza.

**CORONA VS UHABA**

Kaguo anatoa ufafanuzi wa matukio ya uhaba mafuta hivi karibuni, mzizi mkuu ukiwa ni mlipuko wa ugonjwa wa corona uliozuka nchini mwezi Machi, hivyo biashara ilisimamia katika maeneo mengi kitaifa.

Anakiri petroli ilipungua Aprili kwa asilimia saba na wafanyabiashara wengi walipaswa kujipanga kukabiliana nayo, kutokana na uhalisia uliotawala.

"Kutokana na bahati ambayo nchi yetu ilipewa, ugonjwa huo uliisha na biashara zikafunguliwa, mwezi Juni, matumizi yalipanda hadi asilimia saba, lakini mwezi Julai kwa asilimia 12, wakati wanaoagiza huwa wanafanya hivyo miezi miwili ya nyuma.

"Hivyo, asilimia saba iliyopanda Mwezi Juni, ilikuwa ya mwezi wa nne na mfumuko wa biashara ulipofanyika haukuenda na muda wa uagizaji, maana kuna meli ya dharura ya mafuta lita milioni 28 iliingia nchini Julai 13," anaeleza



Mteja akipatiwa huduma ya mafuta kituoni.

Kaguo anasema, mnamo Julai 27 hadi Agosti 3 mwaka huu, iliingia nchini meli nyingime yenye jumla ya lita za mafuta milioni 89.6, ambayo ni ya matumizi siku 20 na Agosti 10, iliingia meli yenye mafuta jumla ya lita milioni 67.

"Yote haya tunafanya ili kuziba pengo ambalo limetokea, pia tumeiagiza PBPA (wakala) iingize meli mbili mwezi ujao ili mafuta yawe yametengamaa na yapo maeneo mengi," anaeleza.

Katika kufanikisha hilo, anajigamba kuwa EWURA kwa kiasi kikubwa inakabili changamoto ya upatikanaji mafuta ya petroli iliyojitokeza mwishoni mwa mwezi uliopita, ikichangiwa na kuchelewa meli.

Anasema, meli hiyo ilicheleweshwa na kasi ya usafishaji wake (refinery) na kuzuka upepo wa baharini - monsoon, uliyofanya meli husika kusafiri kwa kasi ndogo.

"Kutokana na kuchelewa kwa meli hiyo kwa takribani siku saba, kuna uhaba kidogo uliojitokeza katika maeneo machache. Hata hivyo, EWURA ilifanya mawasiliano na kampuni za mafuta kuhakikisha mafuta yanapatikana katika maeneo yote," anasema.

Kwa mujibu wa Kaguo, hali ya usambazaji mafuta kitaifa ya inaridhisha, isipokuwa katika maeneo kadhaa. Hata hivyo anasema, hali ni shwari ya upatikanaji mafuta katika mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, Pwani na Morogoro.

Aidha, hali hiyo shwari anataja Kanda ya Kaskazini; katika mikoa Tanga, Arusha, Kilimanjaro na Manyara na Kanda kati; inayojumuisha Dodoma, Tabora, Singida na Iringa.

Penye uhaba kidogo anakutaja kuwa ni Nyanda za Juu Kusini; Ruvuma, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi katika mji wake wa Mpanda ndio kulishuhuidiwa uhaba zaidi.

**MABADILIKO YA MATUMIZI**

Kaguo anafafanua mwaka jana, matumizi ya petrol yalikuwa wastani wa lita milioni 3.650 kwa siku na uagizaji tangu Januari mwaka huu ulikuwa ukizingatia wastani huo.

Hata hivyo, anasema kuanzia Juni matumizi hayo yameongezeka kufikia lita milioni 3.683 kwa siku na Julai mwaka huu yaliongezeka zaidi kufikia lita milioni 4.425, sawa ongezeko la asilimia 21.

Anasema, namna ya kubadili sasa kuna akiba ya mafuta yanayotosheleza mahitaji nchini. Tangu tarehe 29 mwezi uliopita hadi tarehe 31 mwezi huu, yaani siku 10 zijazo kuna meli tatu zilishawasili zikiwa na jumla ya lita 89.564.

Mafuta hayo kwa ajili ya soko la ndani na zitatosheleza matumizi ya zaidi ya siku 18.

Anafafanua, meli nyingine tatu zilizotarajiwa kuwasili kuanzia Jumatatu kati ya Agosti 17na 31 zikiwa na takribani lita milioni 100.075 zitakazotosheleza mahitaji ya nchi kwa zaidi ya siku 22.

"Mafuta ya dizeli yapo ya kutosha na meli za mafuta hayo zenye jumla ya lita milioni 193.391 zinategemewa kuwasili nchini mwezi Agosti mwaka huu na yatatosheleza mahitaji kwa zaidi ya siku 30,"anasema.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Utitiri wa vyama dhaifu hauna afya katika siasa






NA JOSEPH KULANGWA

KUMESHAPAMBAZUKA tu, kote na katika mchakato wa kutafuta Rais mpya au kuendelea na aliyepo. Ni demokrasia tu ndiyo inayotuhangaisha.

Vinginevyo, tungejisahaulisha, mpaka aliyepo aage dunia ndipo tutafute mwingine. Lakini, tulishakubaliana, hivyo tunapaswa kutekeleza makubaliano.

Mkataba wetu ni kwamba kila baada ya miaka mitano, tunakusanyika kutafuta kiongozi mwingine wa nchi, ama tumwongeze mitano mingine aliyepo au tumweke pembeni aingie mwingine kwa miaka mitano. Na hapatikani mpaka chama chake cha siasa kiwe kimemuidhinisha.

Zamani enzi hizo mambo yalikwa 'bulbul' tu. Kama wewe ni toto la kiume na la kwanza la mtemi au Chifu au Mfalme, moja kwa moja ulijihesabu kukalia kiti cha baba yako na ni pale anapopoteza sifa ya kuongoza, iwe kwa kuaga dunia au amekutwa na janga ambalo halitamuwezesha kabisa kuendelea kukuongozeni.

Na hiyo haikuwa kwetu tu sisi Waafrika, almarufu watu weusi, hata hao Wazungu ambao wanatamba kutuletea ustaarabu, nao walikuwa na mfumo huohuo wa Mfalme au Malkia kurithisha mwanafamilia, ndiyo sababu hadi leo tunaendelea kumsikia Malkia Elizabeth II akiongoza au kutawala huko Uingerezani.

Wabongo hapa tuna vyama 19 vya siasa na vingi hujulikana nyakati za uchaguzi na vyote kwa mujibu wa taratibu na malengo ya chama cha siasa, ni kutaka kuongoza. Ni kutaka kutwaa dola, hivyo vyote kutakiwa kuonana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuomba ridhaa ya kuzunguka mijini na mitaani, vijijini na kwingineko kuomba kura, ili viunde serikali.

Ni hiyari, kwamba chama kinaweza kumsimamisha mmoja wa watu wake kuperusha bendera, ili hatimaye katika uchaguzi baada ya kampeni, kipate ridhaa ya wengi, vivyo hivyo hiyari kwa chama hicho hicho kutosimamisha mtu na badala yake kuamua kushabikia mgombea wa chama kingine.

Inaweza kushangaza, lakini inatokea sisi Wabongo tayari tuna vyama viwili; Tanzania Labour Party (TLP) kinachongozwa na mwanasiasa mkongwe aliyepata kugombea urais, Augustino Lyatonga Mrema na cha United Democratic Party (UDP) cha John Momose Cheyo, ambaye naye aliwahi kuwania ofisi hiyo kubwa vimejikausha.

Vyenyewe viwili hivyo, vinasema vinamuunga mkono mgombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli. Ni uamuzi na demokrasia, kwani viongozi hao wameweza kushawishi wanachama wao na kukubaliana kwa kaulimoja, kuwa mgombea wao ni Dk. Magufuli. Lakini, kila mmoja ataamua Oktoba 28 kwenye sanduku la kura. Sanduku la siri.

Demokrasia ina gharama zake. Demokrasia huamua jambo kwa kupigwa kura, wengi hushinda dhidi ya wachache, ingawa kuna nyakati wachache nao hutakiwa kusikilizwa.

Hivyo, katika vyama hivi, wengi walishinda, lakini si kweli kuwa hao wachache waliobaki, itakuwa rahisi kukubaliana na wengi hata kwenye sanduku la kura.

Kwa kuwa kuunda chama cha siasa mustakabali wake huwa ni kutwaa uongozi wa dola, hivyo ni lazima kusiwe na budi ya chama hicho kilichosajiliwa, kusimamisha mgombea urais, kwa sababu haiwezekani kutwaa madaraka ya nchi, bila ya kuwa na Rais.

Haitoshi tu kuwa na wabunge na hivyo ukapewa fursa ya kuunda serikali, la hasha.

Pengine kwa kuliangalia hili, ndiyo sababu watu wakadai Katiba Mpya ili mambo kama haya yafanyiwe kazi na kama alivyopata kusema marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, ni vema kuwa na vyama vichache imara, kuliko utitiri wa vya madhaifu.

Ni kazi kubwa sana kwa chama kisichosimamisha mgombea urais kupata mbunge, licha ya viongozi wa vyama hivyo mara kadhaa kuomba hisani kwa mgombea mwenye nguvu kuachiwa baadhi ya majimbo.

Hiyo ni jozi ambayo haitakaa itokee, bali kukubali matokeo ya kukosa mbunge na hivyo kubakiwa uanasiasa wa kawaida.

Inafikirisha sana, kwamba kama unachama, lakini hakigombei urais ni yapima lengo yake ya baadaye, pia wanachama wa chama husika wanakuwa na maslahi gani katika chama hicho, ambacho kinaonekana kama kikundi tu cha kufarijiana?

Ni vema chama kikajivunja na kujiunga na kingine 'swahiba'. Hakuna dhambi TLP na UDP kuvunjika au kujivunja na kujiunga na CCM kwa maslahi mapana ya nchi. Alamsiki!

**•Simu: +255 713 410008 nabaruapepe: jkulangwa@yahoo.com**

UCHUMI

# Pata mubashara 'hohehahe' waliowekeza katika 'vigodoro' warekebishwa darasani

## • Watoto wapewa kwa nyayo zilezile za wazazi

Na Beatrice Philemon

UNAPOWAONA baadhi ya kinamama kutoka kaya masikini katika kata ya Keko Mwanga B Wilaya ya Temeke, jinsi walivyo kwa muonekano wao, ni vigumu kuamini uhalisia wa maisha yao ya kila siku.

Wapo ambao fedha wanayoipata kutoka kwenye biashara zao za kila siku hautumiki kwa usahihi, ikiendana na kuendekeza uvivu na starehe, elimu kwao siyo kipaumbele, ilhali kimaendeleo wapo nyuma; masikini na hawajui namna bora ya kujiendeleza, hawajui kusoma na kuandika.

Ingawa kuna baadhi ya wanawake wameamua kufanya biashara ndogo kujiongezea kipato, fedha nyingi ikiangukia katika burudani za 'vigodoro' na safari za kwa waganga wa kienyeji, matokeo biashara zao zinadumaa.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Mtendaji wa shirika lisilo la kiserikali la Women in Social Entrepreneurship (WISE), Dk. Astronaut Bagile, anasema wameingia katika mkakati kusaidia kuwainua kinamama hao waanze kubadilika.

Kwa mujibu wa Dk. Bagile, ni namna inayoweza kuwasaidia kushuka ngazi ya familia na jamii kwa ujumla na hivi sasa WISE inawafundisha elimu ya biashara kinamama wajasiriamali kutoka kaya masikini, wakazi wa Keko Mwanga B na jinsi ya kuweka fedha za akiba.

Anasema kinamama waliopata mafunzo ni wanaitwa 'single mothers' kwa maana ya wengi kutoka kwa wazazi na pale waliko sasa, hawamjui baba wala mume na walijikita katika biashara ndogo kama vile 'mama ntilie', wauza mitumba, vinywaji baridi, karanga, pochi na nguo.

"Mwisho wa siku tunategemea kuona akina mama hawa wanakuwa na ndoto ya kuboresha maisha yao, wanaongeza kipato, samani, wanapanua masoko ya biashara zao, watakuwa na utu na watakuwa na sauti katika jamii na wakati huo huo kuwa mabalozi wa wanawake wengine katika Wilaya ya Temeke," anasema.

Dk. Baglie anaendelea kusema kuwa waliamua kutoa mafunzo hayo baada ya kugundua kuwa wanawake wengi katika eneo hilo, hawana elimu ya biashara.

Ni mafunzo yanayotolewa kwa ubia wa ufadhili kutoka shirika la kimataifa la Holt Children's Services Incorporation ya Korea Kusini, inayowasaidia kinamama kuanzisha, kuboresha na kusimamia biashara na kuvutia vyanzo vingi vya mitaji.

"Kinamama mbadilike! Muache tabia ya kwenda kupeleka fedha zenu kwenye vigodoro kwa ajili ya kutunza wenzenu, pia kwenda kwa waganga wa kienyeji, mkatumie fedha zenu kwenye vitu vya maana, mjifunze nidhamu ya kutunza fedha bila hivyo mtaendelea kuwa masikini," anasema

Anawatahadharisha, kwamba wakiendelea kugawa fedha kwenye 'vigodoro' kwa mbwembwe za 'kutunza' wenzao, ilhali katika maisha yao na pale wakishindwa kumpeleka hospitali.

"Jifunzeni kutunza fedha mnazozipata kutoka kwenye biashara zenu," Dk. Bagile anawashauri kinamama wajitahidi na kujifunza nidhamu ya kufanya alichokusudia kukifanya.

"Sisi tunawasaidia kupata elimu ya biashara, lakini baadaye mtajiweka kwenye vikundi vidogo vigodo, ili muweze kutambulika na hatimaye hata kuanza kupata mikopo midogo midogo, ili kuendesha biashara zenu," anasema mkurugenzi huyo.



Mkurugenzi Mtendaji wa sasa ya WISE, Dk. Astronaut Bagile (aliyesimama), akiwanoa darasani kinamama wa Keko Mwanga, Dar es Salaam. **PICHA: BEATRICE PHILEMON.**

Rai yake ni kuwataka kwenda na anachokitaja 'kukomaa' na ndoto zao dhidi ya umasikini. Anaendelea:"Baada ya mafunzo tutakuja kwenye biashara zenu kuangalia jinsi mnavyofanya biashara.

"Ninaamini kupitia mafunzo haya, mtaweza kupanua mawazo yenu, kuboresha biashara zenu na kuwa mabalozi wa wanawake wengine katika maeneo yenu."

"Katika utafiti wetu tuligundua kuwa kinamama wengi wanaanzisha biashara wakiwa na shida kama njia ya kujikimu katika hali ya kiuchumi matokeo yake biashara zao hazikui, zinadumaa, hazikidhi mahitaji yao na hivyo kuwafanya kuwa masikini na kupoteza matumaini katika biashara zao," anasema.

Dk. Bagile anasema, uzoefu unaonyesha kinamama wengi wanashindwa kukamata soko la bidhaa zao, kulinda, kutunza na hawakopesheki, kwa sababu hawana historia ya kutunza kumbukumbu za biashara hizo na hawatambuliki kwa sababu hawajajisajili.

Anasema, hilo linawafanya waishie kukopa kwa ndugu, rafiki na malikauli yaani, maarufu kutaalamu 'in kind capital' hata kuwakwaza wasifikie ndoto zao kibiashara na waendelee kubaki masikini.

**DARASA WALILOPATA**

Inaelezwa kupitia mafunzo tajwa, kinamama hao wamefundishwa namna ya kutambua na kuchagua wazo bora la biashara, taratibu za kuanzisha, namna ya kuzisimamia, kutambua na kutafuta masoko.

Anasema katika soko hilo walijifunza namna ya kulinda masoko, kukabili ushindani wake, kutangaza biashara zao kwa njia ya kidigitali kwenye mikusanyiko ya watu na kupitia uhusiano waliokuwa nayo marafiki.

Lingine analitaja, walifundishwa namna ya kuanisha vyanzo vya mitaji zaidi wanavyofahamu na masharti ya kupata mikopo, vigezo vinavyowekwa na hizo taasisi za kifedha.

Pia, darasa lilifikia katika upungufu wa kila chanzo cha mikopo, hali inayowawezesha kujipanga ili kupanua wigo wa vyanzo vya mitaji.

Anasema, katika safari ya miaka mitatu waliopanga, wanataka kuwaacha wanawake katika kaya masikini wakiwa bora na wanaishi katika makazi bora, watoto wao wanapata elimu bora, kama ilivyo kwa wananchi wengine.

"WISE itaendelea kuwafundisha ili mkue, mjitahidi kuweka kumbukumbu za kifedha kutokana na biashara mnazozifanya, ili biashara yako ikuonyeshe unakua au la, ili na wewe uweze kubadilika," anasema.

Dk. Bagile anasema kinamama wengi wanashindwa kupata mitaji, kwa sababu hawatunzi kumbukumbu zao, hivyo wanaendelea kuwafundisha ili waweke historia ya kifedha, mahesabu sahihi.

**KINAMAMA**

Mariam Julius anazungumza kwa niaba ya wenzake, akiwaomba kinamama kutoka kaya masikini wabadilike na kuibadika kitabia, kufuata waliojifunza.

"Tulichojifunza tukifanyie kazi, ukiona umekwama mahali mfuate mwenzako mueleze sehemu ambayo hukuelewa atakufundisha.

"Ikishindikana njoo kwa walimu hapa WISE watakuelekeza tena. Walimu wapo kwa ajili yetu, pia tumejifunza mengi, tuwe na umoja na nguvu ya pamoja ili tuweze kuvuka sehemu tuliyopo," anashauri.

Mwezeshaji kutoka shirika lisilo la kiserikali la Women in Social Entrereneurship (WISE), Nshekanabo Njwelige, anashauri kinamama kabla ya kuingia kwenye vikundi kama Vicoba na SACCOS, ni vyema wawe na malengo na mipango sahihi ya pesa.

Anasema: "Tuwekeze zaidi kwenye VICOBA, SACCOs kwa sababu hakuna stress ya kurudisha riba."

Pia anataja maeneo mengine wanayoweza kupata mikopo ni kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Temeke, kwa sababu kila mwaka ina bajeti ya asilimia 10 ya bajeti yake, kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu.

"Halmashauri (Temeke) inatoa asilimia nne kwa wanawake, asilimia nne kwa vijana na watu wenye ulemavu asilimia mbili," anasema Njwelige.

Wadau hao pia walichukua hatua ya kuelimisha watoto walio katika mazingira magumu katika kupata elimu, kwa misaada na elimu ya ziada kwa maana ya tuisheni.

## TEMBO WATATU WAFUNGA MASHINE KUSAGA NA 'KUVUNA' MAHINDI YA WAKULIMA 100

INATOKA UK.11

dhibiti tembo kwa kutumia pilipili anapaswa kutolewa kijijini Ngarambe, Rufiji ili kupunguza migogoro ya tembo na wakulima, inayosaidia kuwaganya tembo wahofu kuvamia mazao.

"Nilipatiwa mafunzo hayo, unachukua pilipili na 'oili' chafu unafunga kwenye kitambaa na kupaka mafuta hayo kwenye kitambaa, kisha unazungusha katika eneo la shamba lako.

"Mbinu hii imiesaidia, kwa sababu tembo anavyokuja katika eneo la shamba, akisikia harufu ya pilipili inamfanya apige chafya, hivyo pilipili hizo zinakuwa kama zinamchoma anapovuta hewa na kuamua kuondoka," anaelezas Mhifadhi Mpunde.

Hata hivyo anasifu, mafanikio kijijini Ngarambe katika mwaka uliopo wa kilimo, kumevunwa tani 20 za mahindi jambo ambalo sio la kawaida.

Anasema, shida iko katika vijiji vya Ngorongo hadi Mloka, ambako kuna matukio endelevu ya tembo kuwatesa na bado hawajapatiwa elimu ya pilipili.

"Kipindi cha kilimo hasa kwenye msimu wa embe ama korosho huwezi kumfukuza tembo. Hii nayo ni changamoto, inafika wakati hata kama embe zimebaki chache, atazunguka na kurudi tena ili mradi azimalize," anaeleza. Pia, anaeleza uzoefu wake kwamba hata wakulima wanapovuna mazao yao na kuyahifadhi ghalani, tembo hubomoa na kula.

"Tembo kumzuia kufika kwenye makazi ni vigumu, maana wanazijua hizo...tumefanikiwa kuwawezesha wananchi kupata mazao yao, lakini sio kumzuia tembo asifike kwa wananchi," anasimulia.

Aidha, anasema wana taarifa zaidi ya watu 100 mazao yao yameliwa na tembo na tayari majina wameyawasilisha katika ngazi husika wapatiwe kifuta machozi.

Mpunde anasema, Idara ya Wanayamapori inakwama majukumu yake kwa kukosa gari na vifaa vya kazi, akifafanua: "Taarifa inafika leo (kutoka Mloka kuna tembo wanasumbua, hatuna magari ya kutuwahisha kufika hicho kijiji kwa wakati wiki inaweza kupita ndio tunaenda."

Anasema huwa wanaazima gari kutoka idara nyinginezo, lakini kwa sasa hakuna magari hayo.

UCHUMI

# Pata mubashara 'hohehahe' waliowekeza katika 'vigodoro' warekebishwa darasani

- Watoto wapewa kwa nyayo zilezile za wazazi

**Na Beatrice Philemon**

UNAPOWAONA baadhi ya kinamama kutoka kaya masikini katika kata ya Keko Mwanga B Wilaya ya Temeke, jinsi walivyo kwa muonekano wao, ni vigumu kuamini uhalisia wa maisha yao ya kila siku.

Wapo ambao fedha wanayoipata kutoka kwenye biashara zao za kila siku hautumiki kwa usahihi, ikiendana na kuendekeza uvivu na starehe, elimu kwao siyo kipaumbele, ilhali kimaendeleo wapo nyuma; masikini na hawajui namna bora ya kujiendeleza, hawajui kusoma na kuandika.

Ingawa kuna baadhi ya wanawake wameamua kufanya biashara ndogo kujiongezea kipato, fedha nyingi ikiangukia katika burudani za 'vigodoro' na safari za kwa waganga wa kienyeji, matokeo biashara zao zinadumaa.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Mtendaji wa shirika lisilo la kiserikali la Women in Social Entrepreneurship (WISE), Dk. Astronaut Bagile, anasema wameingia katika mkakati kusaidia kuwainua kinamama hao waanze kubadilika.

Kwa mujibu wa Dk. Bagile, ni namna inayoweza kuwasaidia kushuka ngazi ya familia na jamii kwa ujumla na hivi sasa WISE inawafundisha elimu ya biashara kinamama wajasiriamali kutoka kaya masikini, wakazi wa Keko Mwanga B na jinsi ya kuweka fedha za akiba.

Anasema kinamama waliopata mafunzo ni wanaitwa 'single mothers' kwa maana ya wengi kutoka kwa wazazi na pale waliko sasa, hawamjui baba wala mume na walijikita katika biashara ndogo kama vile 'mama ntilie', wauza mitumba, vinywaji baridi, karanga, pochi na nguo.

"Mwisho wa siku tunategemea kuona akina mama hawa wanakuwa na ndoto ya kuboresha maisha yao, wanaongeza kipato, samani, wanapanua masoko ya biashara zao, watakuwa na utu na watakuwa na sauti katika jamii na wakati huo huo kuwa mabalozi wa wanawake wengine katika Wilaya ya Temeke," anasema.

Dk. Baglie anaendelea kusema kuwa waliamua kutoa mafunzo hayo baada ya kugundua kuwa wanawake wengi katika eneo hilo, hawana elimu ya biashara.

Ni mafunzo yanayotolewa kwa ubia wa ufadhili kutoka shirika la kimataifa la Holt Children's Services Incorporation ya Korea Kusini, inayowasaidia kinamama kuanzisha, kuboresha na kusimamia biashara na kuvutia vyanzo vingi vya mitaji.

"Kinamama mbadilike! Muache tabia ya kwenda kupeleka fedha zenu kwenye vigodoro kwa ajili ya kutunza wenzenu, pia kwenda kwa waganga wa kienyeji, mkatumie fedha zenu kwenye vitu vya maana, mjifunze nidhamu ya kutunza fedha bila hivyo mtaendelea kuwa masikini," anasema

Anawatahadharisha, kwamba wakiendelea kugawa fedha kwenye 'vigodoro' kwa mbwembwe za 'kutunza' wenzao, ilhali katika maisha yao na pale wakishindwa kumpeleka hospitali.

"Jifunzeni kutunza fedha mnazozipata kutoka kwenye biashara zenu," Dk. Bagile anawashauri kinamama wajitahidi na kujifunza nidhamu ya kufanya alichokusudia kukifanya.

"Sisi tunawasaidia kupata elimu ya biashara, lakini baadaye mtajiweka kwenye vikundi vidogo vigodo, ili muweze kutambulika na hatimaye hata kuanza kupata mikopo midogo midogo, ili kuendesha biashara zenu," anasema mkurugenzi huyo.



Mkurugenzi Mtendaji wa sasa ya WISE, Dk. Astronaut Bagile (aliyesimama), akiwanoa darasani kinamama wa Keko Mwanga, Dar es Salaam. **PICHA: BEATRICE PHILEMON.**

Rai yake ni kuwataka kwenda na anachokitaja 'kukomaa' na ndoto zao dhidi ya umasikini. Anaendelea:"Baada ya mafunzo tutakuja kwenye biashara zenu kuangalia jinsi mnavyofanya biashara.

"Ninaamini kupitia mafunzo haya, mtaweza kupanua mawazo yenu, kuboresha biashara zenu na kuwa mabalozi wa wanawake wengine katika maeneo yenu."

"Katika utafiti wetu tuligundua kuwa kinamama wengi wanaanzisha biashara wakiwa na shida kama njia ya kujikimu katika hali ya kiuchumi matokeo yake biashara zao hazikui, zinadumaa, hazikidhi mahitaji yao na hivyo kuwafanya kuwa masikini na kupoteza matumaini katika biashara zao," anasema.

Dk. Bagile anasema, uzoefu unaonyesha kinamama wengi wanashindwa kukamata soko la bidhaa zao, kulinda, kutunza na hawakopesheki, kwa sababu hawana historia ya kutunza kumbukumbu za biashara hizo na hawatambuliki kwa sababu hawajajisajili.

Anasema, hilo linawafanya waishie kukopa kwa ndugu, rafiki na malikauli yaani, maarufu kutaalamu 'in kind capital' hata kuwakwaza wasifikie ndoto zao kibiashara na waendelee kubaki masikini.

**DARASA WALILOPATA**

Inaelezwa kupitia mafunzo tajwa, kinamama hao wamefundishwa namna ya kutambua na kuchagua wazo bora la biashara, taratibu za kuanzisha, namna ya kuzisimamia, kutambua na kutafuta masoko.

Anasema katika soko hilo walijifunza namna ya kulinda masoko, kukabili ushindani wake, kutangaza biashara zao kwa njia ya kidigitali kwenye mikusanyiko ya watu na kupitia uhusiano waliokuwa nayo marafiki.

Lingine analitaja, walifundishwa namna ya kuanisha vyanzo vya mitaji zaidi wanavyofahamu na masharti ya kupata mikopo, vigezo vinavyowekwa na hizo taasisi za kifedha.

Pia, darasa lilifikia katika upungufu wa kila chanzo cha mikopo, hali inayowawezesha kujipanga ili kupanua wigo wa vyanzo vya mitaji.

Anasema, katika safari ya miaka mitatu waliopanga, wanataka kuwaacha wanawake katika kaya masikini wakiwa bora na wanaishi katika makazi bora, watoto wao wanapata elimu bora, kama ilivyo kwa wananchi wengine.

"WISE itaendelea kuwafundisha ili mkue, mjitahidi kuweka kumbukumbu za kifedha kutokana na biashara mnazozifanya, ili biashara yako ikuonyeshe unakua au la, ili na wewe uweze kubadilika," anasema.

Dk. Bagile anasema kinamama wengi wanashindwa kupata mitaji, kwa sababu hawatunzi kumbukumbu zao, hivyo wanaendelea kuwafundisha ili waweke historia ya kifedha, mahesabu sahihi.

**KINAMAMA**

Mariam Julius anazungumza kwa niaba ya wenzake, akiwaomba kinamama kutoka kaya masikini wabadilike na kuibadika kitabia, kufuata waliojifunza.

"Tulichojifunza tukifanyie kazi, ukiona umekwama mahali mfuate mwenzako mueleze sehemu ambayo hukuelewa atakufundisha.

"Ikishindikana njoo kwa walimu hapa WISE watakuelekeza tena. Walimu wapo kwa ajili yetu, pia tumejifunza mengi, tuwe na umoja na nguvu ya pamoja ili tuweze kuvuka sehemu tuliyopo," anashauri.

Mwezeshaji kutoka shirika lisilo la kiserikali la Women in Social Entrereneurship (WISE), Nshekanabo Njwelige, anashauri kinamama kabla ya kuingia kwenye vikundi kama Vicoba na SACCOS, ni vyema wawe na malengo na mipango sahihi ya pesa.

Anasema: "Tuwekeze zaidi kwenye VICOBA, SACCOs kwa sababu hakuna stress ya kurudisha riba."

Pia anataja maeneo mengine wanayoweza kupata mikopo ni kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Temeke, kwa sababu kila mwaka ina bajeti ya asilimia 10 ya bajeti yake, kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu.

"Halmashauri (Temeke) inatoa asilimia nne kwa wanawake, asilimia nne kwa vijana na watu wenye ulemavu asilimia mbili," anasema Njwelige.

Wadau hao pia walichukua hatua ya kuelimisha watoto walio katika mazingira magumu katika kupata elimu, kwa misaada na elimu ya ziada kwa maana ya tuisheni.

## TEMBO WATATU WAFUNGA MASHINE KUSAGA NA 'KUVUNA' MAHINDI YA WAKULIMA 100

**INATOKA UK.11**

dhibiti tembo kwa kutumia pilipili anapaswa kutolewa kijijini Ngarambe, Rufiji ili kupunguza migogoro ya tembo na wakulima, inayosaidia kuwaganya tembo wahofu kuvamia mazao.

"Nilipatiwa mafunzo hayo, unachukua pilipili na 'oili' chafu unafunga kwenye kitambaa na kupaka mafuta hayo kwenye kitambaa, kisha unazungusha katika eneo la shamba lako.

"Mbinu hii imiesaidia, kwa sababu tembo anavyokuja katika eneo la shamba, akisikia harufu ya pilipili inamfanya apige chafya, hivyo pilipili hizo zinakuwa kama zinamchoma anapovuta hewa na kuamua kuondoka," anaelezas Mhifadhi Mpunde.

Hata hivyo anasifu, mafanikio kijijini Ngarambe katika mwaka uliopo wa kilimo, kumevunwa tani 20 za mahindi jambo ambalo sio la kawaida.

Anasema, shida iko katika vijiji vya Ngorongo hadi Mloka, ambako kuna matukio endelevu ya tembo kuwatesa na bado hawajapatiwa elimu ya pilipili.


"Kipindi cha kilimo hasa kwenye msimu wa embe ama korosho huwezi kumfukuza tembo. Hii nayo ni changamoto, inafika wakati hata kama embe zimebaki chache, atazunguka na kurudi tena ili mradi azimalize," anaeleza. Pia, anaeleza uzoefu wake kwamba hata wakulima wanapovuna mazao yao na kuyahifadhi ghalani, tembo hubomoa na kula.

"Tembo kumzuia kufika kwenye makazi ni vigumu, maana wanazijua hizo...tumefanikiwa kuwawezesha wananchi kupata mazao yao, lakini sio kumzuia tembo asifike kwa wananchi," anasimulia.

Aidha, anasema wana taarifa zaidi ya watu 100 mazao yao yameliwa na tembo na tayari majina wameyawasilisha katika ngazi husika wapatiwe kifuta machozi.

Mpunde anasema, Idara ya Wanayamapori inakwama majukumu yake kwa kukosa gari na vifaa vya kazi, akifafanua: "Taarifa inafika leo (kutoka Mloka kuna tembo wanasumbua, hatuna magari ya kutuwahisha kufika hicho kijiji kwa wakati wiki inaweza kupita ndio tunaenda."

Anasema huwa wanaazima gari kutoka idara nyinginezo, lakini kwa sasa hakuna magari hayo.



# Wizara kuleta mageuzi sekta ya kilimo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawiri, amesema kuwa wizara hiyo imelenga kuendeleza mageuzi katika sekta ya kilimo kwa kuifanya ya kisasa, jumuishi na yenye ushindani.

Alisema kuwa sekta ya kilimo ikijumuisha mazao, mifugo, uvuvi, misitu na rasilimali zisizorejesheka bado inaendelea kuwa ni muhimili mkuu wa uchumi wa Zanzibar.

Alisema hayo Ikulu Mjini Zanzibar wakati akiwasilisha Taarifa ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Mwaka 2019/2020 na wa mwaka 2020/2021.

Alisema sekta hiyo inatoa mchango wa moja kwa moja kwa wananchi katika kujikimu kimaisha na asilimia 40 wameajiriwa na sekta hiyo na inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanategemea sekta hiyo na kwa mwaka 2019 imechangia asilimia 21.2 ya Pato la Taifa. Akieleza kuhusu wizi na uchimbaji holela wa rasilimali ya mchanga, Waziri Mjawiri alisema kuwa wizara kwa kushirikiana na vikosi vya ulinzi vya Zanzibar, imeunda kikosi shirikishi cha doria ambacho kinaendelea kupambana na wizi na uchimbaji wa mchanga kiholela na udhibiti wa ukataji ovyo wa miti.

Alieleza Mpango Kazi wa mwaka 2020/2021 ambao umelenga kuleta Mapinduzi ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kutoka Kilimo duni cha kujikimu kuelekea kilimo endelevu cha kibiashara na chenye tija pamoja na uhifadhi na matumizi. Pia, jumla ya wafanyakazi 263 wameajiriwa ikiwamo wahudumu shambani, maofisa katika ngazi tafauti na wataalamu 68. Dhamira ya wizara hiyo ya kuibadilisha sekta ya kilimo kuwa ya kibiashara ni kwa kuhamasisha ukuaji wa viwanda vidogo, miradi ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu, utumiaji wa teknolojia za kisasa, uzalishaji na usindikizaji wa mazao ya kilimo, kuongeza uzalishaji pamoja na kuweka mazingira bora katika sekta hiyo.

Alisema kuwa wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 inalengo la kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji katika eneo la hekta 65 na kukarabati hekta 87. Alisema pia inatarajia kuongeza uzalishaji wa mpunga kufikia wastani wa tani 50,000 na kuendelea kutoa huduma za matrekta na zana zake kwa wakulima na kufuatilia ukulima wa zao la mpunga katika eneo la ekari 33,800 na mazao mengine ya kilimo. Alisema wizara hiyo pia, itafanya utafiti wa kisayansi, kiuchumi na kijamii kwa mujibu wa 'Zanzibar Research Agenda' kuwajengea uwezo watafiti wa kilimo, mifugo na uvuvi na kuimarisha miundombinu ya utafiti. Naye RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameutaka uongozi wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuendelea kufanyakazi kutokana na kupata mafanikio makubwa.

Dk. Shein alieleza imani yake kwamba zoezi hilo limesaidia kwa kiasi kikubwa kutathmini shughuli za wizara za serikali.

Alisema kuwa serikali imeweka mkazo kufanya utafiti hatua ambayo imesababisha kuanzisha taasisi mbalimbali na kituo cha utafiti cha Kizimbami ndio cha kwanza katika nchi za Afika Mashariki hali inayoonyesha kuwa Zanzibar imepiga hatua muda mrefu.

Alisema taasisi hizo zimeundwa kwa ajili ya kuendeleza kilimo, uvuvi na afya kwa lengo la kuleta tija na Zanzibar itakwenda mbele katika sekta ya kilimo kutokana na programu mbalimbali zinazotekelezwa na wizara hiyo.



Mkurugenzi Idara ya Elimu Sekondari, Asya Iddi Issa, akitoa maelezo kuhusu idara yake, katika kikao cha utekelezaji wa mpango kazi kwa kipindi cha Mwaka 2020/2021 cha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kilichofanyika katika ukumbi wa Ikulu Mjini Zanzibar jana, chini ya Mwenyekiti wake, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein (hayupo pichani). **PICHA: IKULU**

# Naibu Msajili avipongeza vyama kwa uwazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Mohamed Ali Ahmed, amevipongeza vyama vya siasa kwa kufanya uchaguzi wao wa ndani na kuwapata viongozi katika hatua ya awali kwa uwazi na kufuata misingi ya demokrasia ikiwamo baadhi ya vyama kurusha matangazo mubashara.

Akizungumza na wandishi wa habari ofisini kwake Chukwani, alisema wameshuhudia hatua ya awali ya mchakato wa kupata viongozi wa vyama ukifanyika kwa njia ya kidemokrasia ambayo imewaridhisha wagombea na kuondoa malalamiko.

Alisema sheria ya msajili wa vyama vya siasa inavitaka vyama hivyo kuendesha shughuli zao kwa uwazi katika hatua mbalimbali ikiwamo kutafuta viongozi.

Alisema anaamini katika hatua nyingine inayofuata ya kufanya kampeni za kisiasa, viongozi wa vyama hivyo watazingatia maadili, na sheria ikiwamo kufanya kampeni za kistaarabu zenye kuzingatia na kulinda amani na utulivu. Alisema baadhi ya vyama vya siasa mchakato wake wa kupata wagombea nafasi ya urais ulikuwa wazi na kufahamika kwa kila mwanachama mwenye nia ya kugombea nafasi hiyo hadi katika hatua za mwisho ikiwamo za kupigiwa kura.

"Ofisi ya Msajili wa vyama vya siasa Zanzibar imeridhishwa na utendaji wa vyama vya siasa katika mchakato wa awali wa kupata viongozi watakaoshiriki katika hatua mbalimbali za uchaguzi mkuu na matarajio yetu makubwa uchaguzi mkuu ujao utafanyika kwa amani na utulivu," alisema. Alivitaka vyama vya siasa kuzingatia mafunzo waliyopatiwa na Ofisi ya Msajili ikiwamo kuimarisha amani na utulivu na kuzingatia usawa wa kijinsia katika kupata viongozi wa nafasi mbalimbali za uongozi.

Alisema sheria ya Msajili wa Vyama vya Siasa inavitaka vyama kuweka usawa wa kijinsia kwa nafasi za uongozi katika ngazi mbalimbali za juu kuanzia nafasi ya urais, uwakilishi, ubunge na udiwani na kuona kundi la wanawake linashirikishwa na hatimaye kuingia katika vyombo vya uamuzi vya kutunga sheria.

Alivipongeza baadhi ya vyama vya siasa nchini kwa kuonyesha mwelekeo mzuri wa kuzingatia usawa wa kijinsia ikiwamo kuwateua wanawake katika nafasi ya urais, ugombea mwenza pamoja na ubunge na uwakilishi.

"Tunavipongeza baadhi ya vyama vya siasa nchini vimezingatia matakwa ya sheria ya Msajili wa vyama vya siasa vya kutoa nafasi kwa wanawake kugombea nafasi za juu...vipo vyama vya siasa wameteua wagombea mwenza wanawake huku wabunge na wawakilishi wakipewa nafasi zaidi," alisema.

# Samia azitaka redio jamii kutoa elimu udhalilishaji kijinsia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Rais wa Muungano, Samia Suluhu Hassan, amezitaka redio jamii nchini kutoa elimu zaidi kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ambapo baadhi ya tafiti zinaonyesha watoto wa kiume kuathirika vibaya na matukio hayo.

Suluhu alisema hayo huko Binguni Wilaya ya Kati Unguja, wakati akifungua kituo cha redio jamii ambacho ujenzi wake umefadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

Alisema matukio ya vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa jamii ya watoto wa kiume hivi sasa yanasikitisha na kama hakuna juhudi za makusudi za kupambana na athari hizo ipo hatari ya taifa lijalo kizazi kukosa nguvu kazi na uwezo wa kuongoza nchini.

"Nimesikitishwa na taarifa za matukio ya vitendo vya ukatili wa kijinsia ambavyo vimeshika kasi kwa kundi la watoto wa kiume kuharibiwa...tusipochukua tahadhari ipo hatari ya kizazi kijacho kukosa nguvu kazi inayotegemewa," alisema.

Aliitaka jamii ya Wazanzibari kuacha 'muhali' na kutoa taarifa za matukio ya ukatili wa kijinsia kwa taasisi husika ikiwamo jeshi la polisi na kufanyiwa kazi.

Alisema bado wapo wanawake wanaoficha matukio hayo kwa kuwahifadhi waume zao ambao hufanya ukatili wa kutisha katika familia zao kwa kuogopa kupewa talaka.

"Zipo taarifa kwamba wanawake wanaogopa kutoa taarifa za vitendo vya ukatili vinavyofanywa na waume wao katika familia eti kwa kuogopa kupewa talaka," alisema.

Naye Waziri wa Habari Utalii na mambo ya kale, Mahmoud Thabit Kombo, alilipongeza Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi na Utamaduni kwa kusaidia kuendesha vituo vya redio jamii vilivyopo Zanzibar na kusaidia kufikisha ujumbe wa matukio mbalimbali kwa wananchi.

"Tunazo redio jamii nyingi Unguja na Pemba ambazo zimetusaidia kwa kiasi kikubwa kufikisha ujumbe na taarifa za matukio mbalimbali kwa ajili ya ustawi wa jamii na wananchi wetu," alisema.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Shirika la UNESCO nchini, Tirso Do Santos, aliwataka wasimamizi wa redio jamii kuzitumia kutoa elimu ya mambo mbalimbali ikiwamo suala zima la kudumisha amani na utulivu katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu.

"Tunakabiliwa na uchaguzi mkuu wa Oktoba na redio jamii zetu zinatakiwa kufikisha ujumbe wa viongozi na wananchi kudumisha amani na kuepuka vurugu za kisiasa ambazo athari zake ni kubwa," alisema.





# Wanahabari wapewa elimu kupaisha sauti za wanawake, vijana

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAANDISHI wa habari wa mikoa ya Mbeya na Ruvuma wamekubaliana kujikita katika uandishi wa habari unaolenga kupaza sauti za wanawake na vijana hususani wenye ulemavu.

Lengo ni kutimiza ndoto zao ya kuwa viongozi bila kujali hali walizonazo.

Wanahabari waliyasema hayo hivi karibu wakati wa kuhitimisha mafunzo yaliyotolewa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), yaliyolenga kuwajengea uwezo wa namna gani wataweza kutumia kalamu zao kuyasaidia makundi hayo kutimiza malengo yao ya kuwa viongozi katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kuanza Oktoba.

Alisema ni wakati kwa wanahabari kuwapa nafasi wanawake na vijana ambao walishinda na watashinda mchakato wa kura za maoni kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kueleza vipaumbele vyao.

Mmoja wa waandishi kutoka mkoani Ruvuma, Anthony Komba, alisema miongoni mwa maeneo hayajapewa kipaumbele ni kuwapa nafasi watu wenye ulemavu kushindwa kutimiza ndoto zao kutokana na hali walionayo kwanza ni ukata wa fedha na mazingira yaliyopo katika ushiriki.

"Kuna wagombea wengine wanashindwa kutimiza ndoto zao za kuwa viongozi kutokana na hali walizonazo na maeneo wanakotoka hasa vijijini waandishi hatufiki huko mara kwa mara, hivyo kushindwa kupaza sauti hivyo tutajitahidi kufika," alisema Komba.

Mtaalamu wa masuala ya Ufuatiliaji na Tathmini kutoka TGNP, Gratiana Rwakibarila, alisema mafunzo hayo yanalenga kuwapa nafasi wanawake na vijana kupata nafasi ya kueleza yale watakayofanya endapo watapewa ridhaa ya kuwatumikia wananchi wao.

Rwakibarila alisema wanahabari ni daraja kati ya wananchi, serikali na wadau wengine, hivyo wanapaswa kuwapazia sauti ili wananchi wawape nafasi ya kuwaongoza.

"Serikali imejitahidi kuwapa nafasi mbalimbali za uongozi kwa wanawake na vijana na wanafanya vizuri dhamira yetu ya sasa ni kuhakikisha makundi hayo yanaendelea kushika hatamu kwa kuzingatia mlengo wa kijinsia ili kutimiza azma ya 50/50 ya uongozi kati ya mwanaume na mwanamke," alisema Rwakibarila.

# Wazazi watakiwa kuchangia chakula shuleni

**Na Grace Mwakalinga,** MBOZI

WILAYA ya Mbozi mkoani Songwe imewasisitiza wazazi kuendelea kuchangia chakula cha watoto wa shule za msingi kama jitihada za kuboresha mazingira ya ujifunzaji kwa watoto wa shule hizo.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Kaimu Ofisa Elimu Wilaya ya Mbozi, Jason Mlwafu, wakati wa uzinduzi wa ripoti ya utafiti uliyofanywa na TWAWEZA kwa kushirikiana na Shirika la ELIMISHA.

Utafiti ulifanyika mwaka 2017 ili kutathmini uwezo wa watoto kusoma Kiingereza, Kiswahili na Hisabati kwa watoto wenye umri wa miaka 7- 16 katika Wilaya ya Mbozi.

Alisema ili kuongeza ufaulu kwa watoto, wazazi wanapaswa kuchangia chakula shuleni.

Alisema baadhi ya watoto wanaotoka kwenye familia duni, hivyo uwapo wa chakula shuleni utachochea mahudhurio na ufaulu.

Agripina Charles, mmoja wa walioshiriki kufanya tathmini ya ujifunzaji wa watoto wakati wa utafiti huo wilayani Mbozi, alisema walibaini wazazi wengi hawafuatilii maendeleo ya watoto wao, jambo ambalo linachangia kukosa hamasa ya ujifunzaji miongoni mwa watoto.

Alisema takwimu za mwaka 2017 zinaonyesha kwa wilaya kuwa ni asilimia 28.8 tu ya wazazi ambao hujumuika nyumbani kuwaongoza kusoma watoto, wakati wazazi waliofanikiwa kutembelea shule kuongea na walimu kuhusu maendeleo ya watoto ni asilimia 47.7

"Wazazi na walezi walio wengi hawatengi muda wa kufuatilia nini mtoto amejifunza shuleni, wakati tunaendelea na tathmini yetu tulikuwa tunakutana na baadhi ya wazazi wakiwa wanashangaa ambavyo watoto wao wanashindwa kujibu maswali madogo ya kawaida hiyo ilikuwa ishara tosha kuonyesha namna wanavyojitenga na watoto," alisema Agripina.

Akiwasilisha ripoti ya utafiti huo mratibu wa tathmini ya uwezo Debora Mwanyanje alisema watoto wadogo wanatakiwa kupata chakula wangali shuleni, kwani katika maeneo ya vijijini wanatembea umbali mrefu kwenda na kurudi shule ambapo huhitaji nguvu itokanayo na chakula.

Alisema maelekezo ya elimu bila malipo huenda hayakueleweka vema miongoni mwa wazazi na kusababisha baadhi yao wazazi kusitisha kuchangia hata chakula shuleni kwa ajili ya watoto wao.

"Takwimu za mwaka 2017 zinaonyesha mahali pa kuanzia kupima matokeo ya elimu bila malipo kwenye suala la utoaji chakula cha mchana shuleni, ambapo kitaifa ni asilimia 23 tu ya shule za msingi ambazo huwapatia chakula wanafunzi," alisema Debora.

Alisema takwimu zinatuonyesha asilimia 39.9 ya kaya nchini ndizo zinatoa mlo wa asubuhi kwa watoto kabla hawajaenda shule, kati ya wilaya 56 zilizofanyiwa tathmini ya kuangalia kiwango cha uelewa wa kusoma, kuandika na kuhesabu wilaya ya Mbozi ilishika nafasi ya 24 kulingana na vipengele mbalimbali walivyotathminiwa.



Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Uwekezaji, Doroth Mwaluko (kushoto), akishuhudia vijana wa kike wanavyotengeneza mfumo wa umeme wa magari katika karakana ya Kihumbe, alipokuwa katika ziara ya kikazi, jijini Mbeya hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TAKUKURU yaokoa mil. 86/- za AMCOS

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, imeokoa zaidi ya Sh. milioni 86 za vyama vitano vya Ushirika (AMCOS) na Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) zilizokuwa zimetafunwa na viongozi wa vyama hivyo. Mkuu wa TAKUKURU wa Wilaya ya Rungwe, Mohamed Shariff, kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya hiyo, Julius Chalya, walikabidhi fedha hizo juzi kwa viongozi wa vyama hivyo baada ya waliokuwa wamezitafuna kuzirejesha.

Akitoa mchanganuo wa fedha hizo, Shariff alisema Sh. milioni 23.28 zilikuwa za Chama cha Akiba na mikopo cha Kyimo SACCOS, Sh. milioni 51.77 zilikuwa za Kiwira SACCOS na Sh. milioni 7.02 zilikuwa za Ikuti SACCOS.


Vile vile, alisema Sh. milioni 1.11 zilikuwa za Amani Malangali SACCOS na Sh. milioni 2.9 zilikuwa za Chama cha Ushirika cha Isempu AMCOS, ambavyo vyote vilirejeshewa fedha hizo kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao.

"Tunawashukuru wananchi kwa kuendelea kushirikiana na taasisi yetu kwenye mapambano dhidi ya rushwa kwa kutoa taarifa za siri ambazo zinafanikisha kunaswa kwa wahusika, nawaomba wananchi wote kuendelea na utaratibu huu kwa kutupigia kupitia namba zetu za bure," alisema Shariff.

Aliwataka viongozi na wanachama wa AMCOS na SACCOS wanaodaiwa madeni mbalimbali wanatakiwa kurejesha fedha hizo kabla TAKUKURU haijawachukulia hatua. Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Chalya, aliwataka maofisa wa TAKUKURU kuendelea kufuatilia maeneo mengine na kuhakikisha watu wote waliotafuna fedha za AMCOS wanazirejesha ili vyama hivyo viendelee na kazi zao.

Alisema watu wanaotafuna fedha hizo ndio wanaosababisha vyama vingi kufa na wakati mwingine kuanza kuepuka kujiunga na vyama hivyo wakihofia fedha zao kutafunwa na viongozi.

Aliwataka viongozi wa vyama hivyo kuendelea kusimamia kwa uaminifu shughuli za vyama hivyo, ili kila mmoja atamani kujiunga navyo tofauti na ilivyokuwa miaka ya karibuni ambapo vyama vya ushirika vilikufa.



# Ujenzi uwanja Karume kuongeza watalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Balozi Mohammed Ramia Abdiwawa, amesema kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa jengo la abiria la Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume (Terminal Three) kutaongeza mapato na kukuza uchumi. Akizungumza jana katika ziara ya kukagua ujenzi huo, alisema kukamilika kwa ujenzi huo utakuwa na uwezo wa kuchukuwa watu milioni 1.6 na kumaliza tatizo la udogo wa uwanja.

Kutokana na hali hiyo, alisema uchumi wa nchi utakua kutokana na idadi ya wageni watakaoingia nchini.

Alisema biashara ya usafirishaji wa anga imekuwa kubwa duniani, hivyo kukamilika kwa ujenzi huo kutakuza sekta ya utalii.

Pia alisema lengo la kufanya ziara hiyo ni kuangalia fedha zinazotolewa na serikali kama zinatumika ilivyokusudiwa.

"Kutoka na ujenzi unavyoendelea hakuna shaka na matumizi ya fedha. Asilimia 60 ya malipo ya mradi tayari yameshafanywa," alisema.

Meneja ujenzi wajengo hilo, Yasser De Cost, alisema makubaliano ya malipo yameshafanyika kati ya mkandarasi na serikali, hivyo hakuna matatizo yoyote yanayojitokeza na malipo ya fedha hizo yanalipwa kwa mujibu wa makubaliano.

Ujenzi wa jengo la abiria katika uwanja huo wa ndege utakaogharimu Dola milioni 58, unatarajia kukamilika mwishoni mwa mwezi ujao.



Mwenyekiti wa Kamati ya Madawati ya SMZ, Haroun Ali Suleiman (wa pili kushoto), akikabidhi madawati kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, mjini Zanzibar juzi, kwa ajili ya wanafunzi wa madarasa ya maandalizi na msingi.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Walimu wasio na sifa kutopewa leseni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Idrissa Muslim Hija, amesema wizara hiyo kupitia Ofisi ya Mrajis wa Elimu haitatoa leseni kwa walimu ambao hawana sifa za kufundisha.

Alisema walimu watakaopatiwa leseni hizo ni wale wanaofuata maadili, sheria na taratibu zote za ualimu.

Akizungumza jana katika hafla ya utoaji wa leseni za walimu kwa kutumia mfumo wa kielektroniki katika Shule ya Sekondari ya Dk. Ali Mohammed Shein, Raha Leo mjini Zanzibar, alisema ni jambo la msingi kwa walimu watakaopatiwa leseni hizo kuzitumia vizuri kwa kufuata kanuni na masharti yaliyomfanya ikiwamo maadili mema ya ualimu. Dk. Idrissa alisema leseni hizo zimetengenezwa kwa gharama kubwa hivyo ni vyema kuzitunza na kuzihifadhi ili ziendelee kudumu kwa muda mrefu.

"Ni lazima tutunze vizuri kama tunavyotunza vitambulisho vingine vya Mzanzibari, Mtanzania na hata cha kupigia kura," alisema Dk. Idrisa.

Alisema ni wajibu wa walimu kufundisha watoto na kuona wanafanya vizuri katika mitihani yao ya taifa na kipimo cha mwanzo cha mwalimu ni kuona mwanafunzi wake anafanikiwa na anapasi vizuri mitihani yake.

"Tuzitumie leseni hizi kuthibitisha kwamba tunastahiki kupata leseni kwa kuwafanya watoto wetu wasome vizuri na kufanikiwa katika maisha yao," alisema.

Katika hatua nyingine, Dk. Idrissa aliwashauri wanafunzi kusoma kwa bidii na kuacha kupoteza nafasi kwa mambo ambayo hayana maana katika maisha yao ya baadaye.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekuwa ikiweka mazingira mazuri ya kujifunza ikiwamo majengo ya kisasa ya shule, madawati na kutekeleza sera ya elimu bure, hivyo ni wajibu kwa kila mtoto kujikita katika kutafuta elimu ili kuwa viongozi wazuri wa baadaye.

Naye Mkurugenzi Uendeshaji na Utumishi wa Umma, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambaye alikuwa Mrajis wa Elimu, Siajabu Suleiman Pandu, alisema kuanzishwa kwa mfumo huo ni jitihada kubwa za Wizara ya Elimu kuweka utambulisho wa mwalimu na kutambua anatimiza miiko na maadili ya kazi yake.

Alisema imebainika kuwa wapo baadhi ya walimu wanakiuka miiko na maadili ya kazi zao ikiwamo kufanya vitendo vya udhalilishaji kwa wanafunzi jambo ambalo linaweza kurudisha nyuma juhudi za kuleta maendeleo katika sekta ya elimu nchini.

Naye Kaimu Mrajis wa Elimu, Thneyuu Mabrouk Hassan, aliwaomba walimu wa shule zote za Zanzibar kuhakikisha wanalipokea jambo hilo ili kufanikisha ufanisi wa kazi zao za kila siku na kuboresha mapato ya serikali.

## Waziri asema hawajabweteka udhibiti corona

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid Mohamed, amesema serikali haijabweteka na mafanikio ya kudhibiti ugonjwa wa corona.

Alisema wananchi wanaoingia nchini kutoka nchi jirani wanachunguzwa na kupimwa afya zao.

Mohamed alisema hayo jana huko Pemba alipozungumza na wafanyakazi wa hospitali za Chakechake na Wete kwa ajili ya kuwaaga kutokana na kuhitimisha muda wa utumishi wake wa miaka miwili ya kuongoza wizara hiyo.

Alisema Zanzibar imefanikiwa kudhibiti ugonjwa wa corona baada ya kuzingatia na kufuata masharti ya kupambana na ugonjwa huo ikiwamo kupima afya zao na kuweka usafi katika maeneo mbalimbali.

Waziri alisema agizo la Wizara ya Afya la kuwataka wananchi wote wanaoingia nchini kupimwa afya zao liko pamoja na kujitenga kwa kukaa nyumbani kwa muda wa wiki mbili.

"Nachukua nafasi ya kuwapongeza wafanyakazi wa Wizara ya Afya Pemba kwa kufanya kazi kubwa kudhibiti ugonjwa wa corona na kuifanya Pemba kuwa na wagonjwa wachache walioambukizwa," alisema.

Naye Ofisa Mdhamini Wizara ya Afya Pemba, Shadya Shaaban Seif, alisema masharti ya kujikinga na corona yanaendelea kufuatwa kwa mujibu wa maelekezo ya Wizara ya Afya katika vijiji vinavyopakana na maeneo ya mipakani ya Mombasa nchini Kenya.

Alisema hadi sasa hakuna mgonjwa wa corona katika kisiwa cha Pemba ambapo wananchi wanaoingia katika mikoa jirani, ikiwamo Mombasa na Tanga, wanachunguzwa afya zao na kutakiwa wajiweke karantini wenyewe.

"Tumepata mafanikio makubwa katika kudhibiti ugonjwa wa corona ambapo hadi sasa hakuna mgonjwa aliyelazwa katika hospitali kuu tatu zilizopo Pemba na utaratibu wa kuchunguza afya kwa watu wanaoingia Pemba kutoka mikoa jirani bado upo na unafuatwa," alisema.

Baadhi ya asasi za kiraia nchini zimeipongeza Wizara ya Afya kwa mafanikio yake makubwa katika kudhibiti na kupambana na ugonjwa wa corona ambao ulisababisha taharuki na athari kubwa za kiuchumi.

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MATANGAZO MCHANGANYIKO

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**
**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.

### NYUMBA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA, Nyumba ya Gorofa 1, inauzwa na fremu za biashara, umeme na maji. Inafaa kwa kuishi na kwa biashara. Mawasiliano: 0757 079057.**

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

### KUPOTEA KWA CHETI



115865502

**Dr. Janet Bernice Bihondwa** anatangaza kupoteza cheti cha kumaliza kidato cha nne chenye index namba T218-0051,Cheti hiki kilichotolewa na NECTA mwaka 1972. Kwa yoyote atakayeokota atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi au aviwasilishe kwa mhusika.
Polisi Taarifa: **DAR/OST/RB/604165/2020.**

### KUPOTEA KWA CHETI



215865302

**Hussein Suleimani Lugazo** anatangaza kupotea kwa chati cha kidato cha nne chenye index namba **0134/60** kiliichotolewa na Baraza la Mithihani la Tanzania mwaka 1977 katika shule ya Sekondari Moshi . Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **MOR/RB/10085/2016**

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**DEZO CIVILO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina FUSO yenye namba za usajili **T 166 ABN** Chassis no. **FK418750022,** Engine no. **6D17700924.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/586754/2020.**

115866302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2.**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;196/2020**

**Ombi la GODFREY ANGOLWISYE PILLA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ANGOLWISYE ANYUSISYE PILLA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 21/08/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 23/07/2020.

Tarehe 23/7/2020

Sahihi ya Hakimu

115866002

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI**

**INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB:**

**+255 - 0782253676**

### KUPOTEA KWA CHETI



215865202

**Tunu T. Sanga** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1344-0125** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Tanzania mwaka 2018 katika shule ya Sekindari Mwalimu JK Nyerere. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **KIL/RB/2144/2020**

### KUPOTEA KWA CHETI



115865402

**Asupya Nalingigwa** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S347/0558** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Tanzania mwaka 1997 katika shule Tambaza High School. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **DAR/SEL/RB/602464/2020**

***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Obama 'amshambulia' Rais Trump

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS mstaafu wa Marekani, Barack Obama amemshutumu Rais wa nchi hiyo, Donald Trump kwa kuchukulia urais kama onyesho la kipindi cha televisheni, katika hotuba aliotoa kwenye kongamano la chama cha Democrat.

Obama alisema kuwa Rais aliyemrithi wa chama cha Republican hajapata uzoefu wa kazi ya urais kwa sababu hawezi.

Akiwa Ikulu ya White House, Rais Trump alijibu na kusema kuwa yeye alichaguliwa kwa sababu ya hofu Bwana Obama alioacha Marekani.

Katika mkutano wa tatu wa chama cha Democrat, Kamala Harris alikubali uteuzi wake kama makamu wa rais.

Katika kilele kamili cha kongamano hilo la siku nne, mgombea urais kwa chama cha Democrat, Joe Biden alitoa hotuba yake.

Wachambuzi wa masuala ya siasa Marekani wanasema tiketi ya Biden- Harris itakua ni ushindani dhidi ya Rais Trump na makamu wa rais Mike Pence katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Novemba 3.

Mlipuko wa ugonjwa wa corona umelazimisha chama cha Democrat kuachana na mbwembwe na shamrashamra ambazo hutokea wakati wa mikutano ya aina hiyo, na kulazimika kufanya mkutano kupitia mtandao.

Obama alitoa shambulio lake kali zaidi dhidi ya Rais Trump, akizungumza moja kwa moja kutoka Jumba la kumbukumbu ya Mapinduzi ya Marekani huko Philadelphia.

Kwenye hotuba yake, Obama alisema: "Hajaonesha (Rais Trumo) chochote cha kutia bidii katika kazi yake. Hajaonyesha nia ya kupata makubaliano. Hajaonyesha nia ya kutumia nguvu za ofisi hiyo kusaidia yeyote zaidi ya yeye mwenyewe na rafiki zake".

Alisema: "Hana nia yoyote ya kuchukulia urais zaidi ya kama kipindi kingine cha televisheni ambacho anaweza kukitumia kupata umaarufu anoutaka sana".

Amesema kuwa athari za urais wa Trump zimekuwa, msukumo wetu mbaya zaidi kujitokeza, ufahari na sifa zetu kote ulimwenguni zimepotea vibaya, na taasisi zetu za kidemokrasia zimetishiwa jinsi haijawahi kutokea awali.

Obama alizungumzia matukio mengi, ubinafsi, ukosefu wa ubinadamu na nadharia za uwongo".

Alisema: "Musiwaruhusu wachukue nguvu yenu, akasihi wapiga kura wa Marekani. Musiwaruhusu wachukue demokrasia yenu."

Baada ya kueleza hayo, Obama aliwahimiza wapiga kura kumchagua aliyekuwa makamu wa Rais Biden ambaye amesalia na siku 76 zijazo -huku akimsifu kuwa rafiki yangu na 'ndugu yangu.

Kulingana na shirika la habari la Associated Press, vyanzo vya karibu na Obama vinasema kuwa anamuunga mkono kikamilifu Biden, lakini ana wasiwasi kuhusu ushiriki kati ya wapiga kura vijana na haswa wapiga kura.

*BBC*



Wanajeshi wa Mali wakiwa mtaani kuimarisha ulinzi baada ya kutokea kwa mapinduzi ya kumwondoa madarakani Rais Ibrahim Keita.
**PICHA: ALLIANCE**

# Mpinzani wa rais Putin yuko mahututi

**MOSCOW, Urusi**

MKOSOAJI na mpinzani mkubwa wa Rais wa Urusi, Vladmir Putin, yuko katika hali mbaya baada ya kuugua ghafla kutokana na kile kinachoshukiwa kuwa amenyweshwa sumu akiwa kwenye ndege.

Alexei Navalny amelazwa katika kitengo cha wagonjwa mahututi baada ya kuzimia akisaidiwa na mashine ya kupumua.

Alexei Navalny, mkosoaji mkubwa wa muda mrefu wa Rais Putin anapigania uhai wake hivi sasa baada ya kuugua akiwa kwenye ndege akisafiri kuelekea mjini Moscow kutoka mji wa Tomsk ulioko Siberia.

Msemaji wake aliyetoa taarifa alisema Navalny (44) aliugua kutokana na kile kinachoshukiwa kuwa sumu, na alipelekwa hospitali baada ya ndege aliyokuwamo kulazimika kutuwa kwa dharura katika eneo la Omsk.

Kira Yarmysh aliandika ujumbe kwenye ukurasa wa mtandao wa kijamii wa Twitter akisema: "Navalny amezimia na yuko katika hali mahututi".

Msemaji huyo pia aliiambia Redio Echo Moskvy kwamba Navalny alikuwa akitokwa jasho jingi akiwa kwenye ndege na alimuomba amuongeleshe ili aweze kuendelea kuwa na fahamu ya kinachoendelea na baadae alikwenda msalani na kuzimia.

Yarmysh akaongeza kusema kwamba mwanasiasa ni lazima alikunywa kitu kilichotiwa ndani ya chai mapema asubuhi alipokuwa katika mgahawa mmoja kwenye uwanja wa ndege kabla ya kupanda ndege hiyo.

Naibu Mganga Mkuu wa hospitali wa Omsk. Anatoliy Kalinichenko, aliwaambia waandishi wa habari kwamba Navalny yuko katika hali mahututi lakini iliyothibitiwa na madaktari wanafikiria kufanya vipimo mbalimbali. Alisema madaktari walimweleza kuwa sumu iliingia haraka kwenye mwili kutokana na kinywaji cha moto.

*DW*

## Mapinduzi Mali yalaaniwa ndani, nje ya Afrika

**BAMAKO, Mali**

IKIWA imepita siku moja baada ya kutokea kwa mapinduzi nchini Mali ya kumuondoa madarakani Rais wa nchi hiyo, Ibrahim Boubacar Keita, kitendo hicho kimelaaniwa na watu mbalimbali.

Juzi wanajeshi walioasi waliangusha serikali ya Rais Keita na kusababisha Rais huyo kutangaza kujiuzulu.

Msemaji wa wanajeshi hao waasi ameeleza kuwa wamechukua hatua hiyo ili kuiepusha Mali kutumbukia katika vurumai kubwa zaidi.

Alisema sababu ya kuipindua serikali ni kurejesha utulivu na kusimamia kipindi cha mpito cha kuelekea kwenye uchaguzi katika muda utakaofaa.

Hata hivyo hatua ya wanajeshi hao waasi imelaaniwa mara moja na viongozi wa kanda yote ya Sahel, Umoja wa Afrika (AU), Umoja wa Ulaya (EU) na Umoja wa Mataifa (UN).

Waziri wa Mambo ya Nje wa Niger iliyomo kwenye jumuiya ya Kiuchumi ya nchi za Afrika Magharibi, ECOWAS, Kalla Ankourao, alisema amesikitishwa na hatua iliyochukuliwa na wanajeshi wa Mali ya kumwangusha Rais Keita.

Waziri huo alisema kwamba kwa muda wa miezi miwili wamekuwa wanajaribu kusuluhisha na walitumai kwamba watu wa Mali wangezifuata kanuni za jumuiya ya ECOWAS ambazo ni za demokrasia na utawala bora, lakini kuangushwa serikali kumeyakomesha mazungumzo hayo kwa njia ya kikatili.

Waziri huyo wa Niger ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa Ecowas, alisema wanajeshi wa Mali walichukua hatua hiyo wakati mbaya.

Alieleza kuwa nchi za ECOWAS zilihitaji muda ili kuweza kuyashughulikia matatizo ya kina kirefu katika uongozi wa nchini Mali. Alisema nchi hizo zilikuwa zinakaribia kupata suluhisho.

Mwezi uliopita Jumuiya ya kiuchumi ya nchi za Afrika Magharibi ilipendekeza kuundwa serikali ya umoja wa kitaifa ya kuahidi kuendelea kumsaidia Rais Keita, lakini pendekezo hilo lilitupiliwa mbali na wapinzani.

Jumuiya ya ECOWAS yenye nchi wanachama 15 imesema itafunga mipaka yake ya ardhini na ya angani kwa Mali na imesema itasisitiza kuwekwa vikwazo dhidi ya wanajeshi walioipindua serikali. Mali pia itasimamishwa kushiriki kwenye taasisi za uamuzi za jumuiya hiyo ya kiuchumi ya nchi za Afrika Magharibi.

Baraza la Usalama la UN litaitisha kikao cha dharura kuujadili mgogoro wa Mali. Ufaransa na Niger zimeomba kuitishwa kikao hicho.

**DW**

# DE JONG
## NGUZO YA KOEMAN BARCA

**BARCELONA, Hispania**

RONALD Koeman amekataa kuzungumzia kuhusu majaliwa ya Philippe Coutinho, lakini amebainisha Frenkie de Jong atakuwa mmoja wa nguzo katika muonekano mpya wa Barcelona.

Coutinho amebakia kuwa mchezaji aliyesajiliwa kwa ada ya rekodi kubwa na klabu hiyo ya La-Liga, lakini ameshindwa kuonyesha kiwango chake baada ya kutua hapo akitokea Liverpool, na kumfanya apelekwe kwa mkopo kule Bayern Munich.

Hata hivyo, Coutinho aliiadhibu Barca kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati Bayern ikiibuka na ushindi wa mabao 8-2 na kusababisha Quique Setien kufukuzwa.

Koeman alithibitishwa kuwa kocha mpya wa kikosi hicho Jumatano na raia huyo wa Uholanzi, alipewa kazi kubwa ya kukijenga kikosi hicho pale Camp Nou.

Kama ilivyo, Coutinho anatarajia kurudi kwenye kikosi hicho kwa msimu mpya wa 2020-21 na alikuwa akihusishwa mno na uwezekano wa kuhamia kule Arsenal, na nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, anaweza kuwa sehemu ya mipango ya kocha huyo mpya.

"Yeye ni mchezaji wa Barcelona na kama kuna uamuzi utafanywa na wao," alisema Koeman wakati akizungumza na waandishi wa habari alipoulizwa kuhusu Coutinho.

"Kwa sasa nitakuwa na muda zaidi wa kuwaangalia wachezaji vijana hapa. Ni muda wa kuwapa vijana nafasi. Hatuna shaka yoyote ya kuwapa vijana nafasi kama wanastahili."

Wakati Koeman alikataa kumzungumzia sana Coutinho, hakuwa na shaka kuweka wazi kwamba De Jong atakuwa mmoja wa wachezaji vijana watakaopewa nafasi kubwa.

"Kwa mchezaji ambaye anakuja Barca, mwaka wake wa kwanza unakuwa mgumu sana," alisema Koeman akimzungumzia De Jong.

Na kuongeza kwamba, anaamini De Jong atakuwa msaada mkubwa katika kikosi hicho katika msimu wake wa pili.

## GNABRY ANAKARIBIA DARAJA LA JUU –FLICK

**LISBON, Ureno**

HANSI Flick anaamini Serge Gnabry anakaribia kuwa mchezaji wa daraja la juu baada ya straika huyo kufunga mara mbili na kuipeleka Bayern Munich kwenye fainal ya Ligi ya Mabigwa Ulaya.

Gnabry alifunga mabao mawili katika kipindi cha kwanza, kabla ya Robert Lewandowski kufunga la tatu wakati Bayern wakipata ushindi wa 3-0 dhidi ya Lyon kwenye nusu fainali ya mashindano hayo, Jumatano.

Raia huyo wa Ujerumani amefunga mabao 23 katika mechi 45 msimu huu na Kocha Mkuu wa Bayern, Flick anahisi Gnabry anakaribia kuwa mchezaji bora duniani.

"Bao la ufunguzi alilofunga lilikuwa la kuvutia, namna alivyomalizia imemfanya kuwa mmoja wa wachezaji bora," alisema Flick akiwaambia waandishi wa habari.

"Na kama ukiangalia kwenye maendeleo yake si tu kwa Bayern Munich, lakini pia kwa timu ya taifa na hapo unaweza kusema kwa urahisi tu anakaribia kuwa mchezaji wa daraja la juu.

"Ni mchezaji wa aina yake na ni hatari zaidi anapokuwa jirani na goli na tuna furaha kubwa kwamba alifunga mabao mawili."

## UNITED WAAMBIWA WAMSAJILI HAALAND, KANE SI SANCHO

**LONDON, England**




STEVE McClaren amewaambia Manchester United kuwekeza zaidi mkazo wa kuwasajili, Erling Haaland na Harry Kane badala ya Jadon Sancho.

Man United kwa muda mrefu wamekuwa wakimuwania Sancho, huku klabu yake ya Borussia Dortmund mara kwa mara ikisema kwamba haina mpango wa kumuuza winga huyo wa timu ya Taifa ya England.

Jumapili iliyopita, Man United ilichapwa 2-1 na Sevilla kwenye nusu fainali ya Ligi ya Europa, huku safu yao ya ushambuliaji ikikosa nafasi nyingi kwenye kufunga mabao jambo linalomfanya McClaren, aliyewahi kuwa kocha msaidizi wa timu hiyo chini ya Sir Alex Ferguson kuwataka wasajili namba 9 badala ya winga kama Sancho.

"Wale wachezaji wanne pale mbele wapo haraka sana, wapo vizuri na wamekuwa wakisababisha matatizo mengi sana kwa mabeki wa timu pinzani. Hata Anthony Martial naye amekuwa na kiwango kizuri," alisema McClaren.

"Lakini, kwenye mechi kubwa wanaonekana kuwa na tatizo, hawaonekani kama ni wafungaji wa kweli.

"Wanahitaji wachezaji wa daraja la juu kwenye nafasi hiyo. Sidhani kama Lukaku angefiti kwenye kikosi cha Man United, hivyo wanahitaji mtu kama (Erling) Haaland ambaye ndio atawafaa zaidi.

Haaland ndiye mchezaji ambaye McClaren anataka asajiliwe Man United badala ya Sancho na kama ikishindikana basi wavamie Tottenham Hotspur kwenda kumsajili Kane.



# NIACHIENI

## MESSI BARCA - KOEMAN

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi atakuwa kwenye moyo wa mipango ya Ronald Koeman kwa muda mrefu kama "mchezaji bora duniani" akitumaini atabakia hapo Camp Nou.

Koeman alitangazwa kuwa mrithi wa Quique Setien Jumatano, akitarajiwa kwenda kuijenga Barca mpya baada ya kunyanyaswa kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kichapo cha mabao 8-2 kutoka kwa Bayern Munich.

Mkurugenzi wa michezo, Eric Abidal aliondoka baada ya kufukuzwa kwa Setien, ingawa ripoti kwamba Messi anafikiria kuondoka klabuni hapo zilileta mawimbi makubwa.

Rais ambaye amekalia kuti kavu, Josep Maria Bartomeu aliiambia televisheni ya Barcelona kwamba, Messi atakuwa sehemu ya mipango ya klabu hiyo, licha ya kubainisha kwamba hakuzungumza na mchezaji huyo baada ya kichapo cha Barcelona.

Ilitarajiwa kwamba Messi atakuwa mjadala mkubwa wakati Koeman atakapokutana na waandishi wa habari kwa mara ya kwanza baada ya kuchukua nafasi ya ukocha wa klabu hiyo akiiacha ile ya timu ya Taifa ya Uholanzi.

"Messi ni mchezaji bora duniani na unapenda kuwa na mchezaji bora wa dunia kuwa kwenye timu yako," alisema.

"Sijui kama nitatakiwa kumshawishi yeye kubaki. Ningependa kufanya naye kazi kwa sababu anashinda mechi ukiwa naye, nitafurahi kama atabaki."

## ARTETA: ARSENAL ITAKUWA NA HAMASA KUBWA

**LONDON, England**

MIKEL Arteta anatambua akili ya wachezaji wake inatakiwa kuwa na hamasa kubwa kuelekea msimu wa 2020-21, baada ya Arsenal kushinda taji la FA.

Arteta alichukua mikoba ya kuinoa timu hiyo kutoka kwa Unai Emery Desemba na alianza vema mwanzo wake pale kwenye dimba la Emirates.

Alishinda mechi 16 kati ya 28 kwenye mashindano yote, ingawa alishuhudia Arsenal ikimaliza nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

Hata hivyo, Arteta alimaliza msimu akiwa na taji baada ya kuifunga Manchester City 2-0 kwenye nusu fainali ya FA na baadaye fainali kuibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Chelsea. Alipoulizwa kuhusu wapi Arsenal itakuwa msimu ujao, Arteta alijibu: "Ni swali lisilowezekana.

"Sijui hata wapi tutakuwa katika siku ya kwanza ya mandalizi ya msimu mpya. Nawaangalia wachezaji, namna watakavyorudi kutoka likizo, namna gani wanarudi baada ya kushinda, nataka kuona mwamko wao.

"Unajua, kwa kiasi fulani watakuwa wamejiachia kwa sababu tumefanya kitu fulani, lakini nitawaangalia kwanza.

"Tunatakiwa kwenda hatua ya juu zaidi, tunatakiwa kuwa bora zaidi na kujiimarisha wenyewe na kuwa na ari kubwa ya kupata kitu kingine kwa msimu unaokuja."



## INTER, SEVILLA NI VITA FAINALI EUROPA LEO

**COLGNE, Ujerumani**

FAINALI ya Ligi ya Europa inapigwa leo Ijumaa wakati Inter Milan itakapoivaa Sevilla katika dimba la RheinEnergieStadion nchini Ujerumani.

Inter Milan ilitinga hatua ya fainali baada ya ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Shakhtar Donetsk kwenye mchezo wa hatua ya nusu fainali.

Nyota ya mshambuliaji wa zamani wa Manchester United, Lukaku imekuwa kali kwani alifunga mabao mawili sawa na Martinez huku moja likifungwa na D'Ambrosio.

Inakutana na Sevilla ambayo ilishinda mabao 2-1 mbele ya Manchester United ya England ambayo ilikuwa inapewa nafasi kubwa ya kubeba taji hilo.

Kwa Inter Milan inakuwa ni mara ya 10 kutinga hatua ya fainali ya Kombe la Europa huku kibarua cha Kocha Mkuu, Antonio Conte kikiwa kimeshikiliwa kwa muda kwa kuwa inaelezwa kuwa anaweza kutimuliwa ikiwa hatashinda taji lolote msimu huu.

Sevilla ni mabingwa wa kihistoria wa mashindano hayo, wakiwa wameshawahi kulitwaa mara tatu mfululizo.

Inter imetinga michuano ya Ulaya kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2010 ilipobeba mataji matatu likiwamo la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LEWANDOWSKI AINGIA KWENYE HISTORIA UEFA

●●●Sasa amefunga katika mechi tisa mfululizo za Ligi ya Mabingwa Ulaya, ni Ronaldo pekee...

**LISBON, Ureno**

BAO la kichwa la Robert Lewandowski alilofunga wakati Bayern Munich wakiibuka na ushindi wa 3-0 kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Lyon, limempa nafasi ya kuwa kwenye historia ya mashindano hayo.

Lewandowski sasa ameingia kwenye historia ya mashindano hayo makubwa zaidi kwa ngazi ya klabu barani Ulaya, sambamba na Cristiano Ronaldo.

Lilikuwa bao la 15 kwa straika huyo wa kimataifa wa Poland katika mashindano hayo msimu huu, ikiwa ni sehemu ya mabao yake 55 aliyofunga kwenye michuano yote msimu huu.

Ronaldo ndiye mchezaji pekee kwenye rekodi ya kufunga mabao mengi katika mashinano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu mmoja na akifanya hivyo katika msimu mitatu wakati akiwa anacheza pale Real Madrid.

Katika msimu wa 2013-14, mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or alifunga mabao 17, huku akifunga 16 na 15 katika msimu wa 2015-16 na 2017-18.

Lewandowski sasa amefunga katika mechi tisa mfululio za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ni Ronaldo pekee mwaka 2018 alifunga katika mechi 11 mfululizo pamoja na mchezaji wa zamani wa Manchester United, Ruud van Nistelrooy ambaye alifunga katika mechi tisa mfululizo mwaka 2003.

## KWA UFUPI

**MOURINHO KUMREJESHA BALE**
JOSE Mourinho anataka kumrejesha, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 31 katika klabu ya Tottenham Hotspur kutoka kule Real Madrid. ***(Cuatro)***

**SILVA APEWA OFA CHELSEA**
MLINZI wa kati wa Paris St -Germain, Thiago Silva mwenye umri wa miaka 35, ambaye anaondoka kwenye klabu hiyo ya Ufaransa baada ya fainali za michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, amepewa ofa ya kujiunga Chelsea ***(Telegraph).***

**SANCHO BASI TENA UNITED**
KUSHINDWA kufikiwa makubaliano ya maslahi binafsi ya mkataba wa Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20, kumeongeza ugumu wa uhamisho wake kutoka Borussia Dortmund kwenda Manchester United. ***(ESPN)***

**GREALISH, ROMERO KUPISHANA**
MANCHESTER United wanaweza kuwapatia Aston Villa mlinda mlango, Sergio Romero mwenye umri wa miaka 33, kama sehemu ya makubaliano ili kumpata kiungo wa kati, Jack Grealish mwenye umri wa miaka 24. ***(Mail)***

**CHELSEA, ATLETICO KWA FEDERICO**
KLABU ya Chelsea na Atletico Madrid zinamuwania winga Federico Bernardeschi mwenye umri wa miaaka 26, anayekipiga Juventus. ***(Calciomercato-in Italian).***

**LIVER KUMUUZA MARKO, WILSON**
LIVERPOOL inajiandaa kumuuza kiungo wake, Marko Grujic mwenye umri wa miaka 24 na winga Harry Wilson, 23, msimu huu ***(Mirror).***

**KAI KUTUA CHELSEA WIKI HII**
CHELSEA watakamilisha kumsajili kiungo wa kati wa Ujerumani, Kai Havertz mwenye umri wa miaka 21 wiki hii, kwa mkataba wa miaka mitano iwapo wao na Bayer Leverkusen wanaweza kupunguza tofauti ya pauni milioni 18 ya thamani ya mchezaji huyo. ***(Telegraph)***

**PEREIRA LULU BENFICA, VALENCIA**
KIUNGO wa kati wa Manchester United, Andreas Pereira mwenye umri wa miaka 24, anawaniwa na Benfica na Valencia. ***(ESPN)***

**UNITED KUMREJESHA SANDRO**
MANCHESTER United imerejesha shauku yao kwa beki wa kushoto, Alex Sandro mwenye umri wa miaka 29, anayeichezea Juventus ***(Calciomercato)***

**LEEDS YATAKA WHITE**
LEEDS United imetoa ofa ya tatu inayoaminika kuwa takribani pauni milioni 25 kwa ajili ya kumsajili Ben White mwenye umri wa miaka 22. ***(Sky Sports)***

**SPURS KUMSAJILI BREWSTER**
KLABU ya Tottenham Hotspur inataka kumsajili mshambuliaji wa Liverpool, Rhian Brewster mwenye umri wa miaka 21 kwa mkopo. ***(Football Insider)***



# ONYANGO: MNAONIITA MZEE SUBIRINI LIGI IANZE

**Na Saada Akida**

WAKATI mashabiki wa soka hususan watani wa Simba, Yanga wakiibeza klabu hiyo kuwa imesajili beki 'mzee', Joshua Onyango, mwenyewe ameibuka na kuwatahadharisha wanaombeza kwa kuwaambia "subirini" Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa ianze, mtanyamaza wenyewe.

Tangu kusajiliwa kwa beki huyo wa kimataifa wa Kenya, aliyemaliza mkataba na Gor Mahia ya kwao, mashabiki husuan wa Yanga wamekuwa wakiibeza Simba kwa kusajili mzee.

Lakini Onyango akizungumza na gazeti hili jijini juzi, alisema hatishwi na maneno ya wanaomkejeli kwa kudai kwamba umri wake umeenda wakati hawajaona kasi na uwezo wake uwanjani.

Alisema amekuja kufanya kazi na atahakikisha wale wanaomkejeli na kubeza uongozi wa timu yake umesajili wazee atawafunga midomo juu ya umri wake.

"Nimekuja kufanya kazi Simba, wale wanaojadili umri wangu kwa sasa watanyamaza na watajutia kauli zao, kwa kazi nitakayoonyesha uwanjani," alisema Onyango.

Alisema alipokuwa Kenya katika Klabu ya Gor Mahia alihitaji kupata changamoto mpya baada ya mkataba wake kumalizika na kupata dili la kuwatumikia mabingwa wa Tanzania Bara, Simba, hivyo mashabiki wasubiri wataona kazi yake.

"Wanaosema umri wangu kwa muda huu wanakosea sana, naomba wasubiri kuona nitakachokifanya uwanjani kinaendana na umri wangu au la.

"Suala la kupata nafasi katika kikosi cha kwanza halina tatizo, nina imani kwa sasa itakuwa ngumu, lakini nitapambana katika mazoezi kufanya vizuri ili kuhakikisha nina mshawishi kocha kunipa nafasi ya kuonyesha uwezo wangu," alisema Onyango.

Onyango anaweza kuonekana uwanjani Jumamosi kwa mara ya kwanza kuitumikia klabu hiyo kama Kocha Mkuu, Sven Vandenbroeck atashawishika kumpanga wakati Simba itakapoivaa Vital'O ya Burundi kwenye mechi ya Simba Day itakayopigwa Uwanja wa Taifa kabla ya kwenda Arusha kumenyana na Namungo FC katika mchezo wa Ngao ya Jamii.

## UFANYE KWELI...




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Mohammed "Mo" Dewji (kulia), akimkabidhi msanii wa muziki, Diamond Platinumz jezi ya mabingwa wa nchi kwa ajili ya kutumbuiza kwenye Tamasha la Simba Day Jumamosi Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam. Diamond ametoa wimbo maalum wa Simba ulioanza kuchezwa jana. **MPIGAPICHA WETU**

# ZFF yafungua dirisha la usajili Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limefungua dirisha la usajili na uhamisho wa wachezaji kwa msimu wa 2020/21 rasmi kuanzia jana na likitarajiwa kufungwa Septemba 19, mwaka huu.

Dirisha hilo la usajili limefunguliwa kwa timu za Ligi Kuu ya Zanzibar kwa upande wa wanaume, Ligi Kuu ya Wanawake, Ligi ya Mikoa pamoja na Ligi za Wilaya.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Mkurugenzi wa Mashindano wa ZFF, Ali Mohmmed Ameir, alisema msimu huu klabu zitasajili kwa njia ya kielektroniki badala ya njia ya analogia (kujaza fomu kwa mkono) kama ilivyozoeleka kwa misimu ya iliyopita.

Alisema ingawa kwa sasa njia hiyo italeta changamoto kwa baadhi ya klabu, lakini shirikisho hilo litazidi kutoa elimu ili kila klabu iweze kufanya usajili kwa wakati kwa kutumia njia ya kielektroniki.

Aidha, azivitaka klabu kufanya usajili kwa wakati uliowekwa na ZFF ili kuepusha usumbufu ambao unaweza kujitokeza mara kwa mara katika kipindi hiki husuan kwa baadhi ya timu kushindwa kusajili kwa wakati.

"Kuna baadhi ya timu zinachelewa kwa makusudi kusajili kwa wakati, utakuta wanasubiri kujua timu nyingine kaachwa mchezaji gani ndipo ianze kusajili, ZFF haitaongeza muda wa ziada kutokana na msimu kuchelewa kumalizika kwa changamoto nyingi ikiwamo mlipuko wa virusi vya corona uliosababisha ligi kusimama," alisema.

Hata hivyo, alizitaka klabu kuhakikisha nakala za mikataba ya wachezaji wao wanaziwasilisha ZFF ili kupunguza changamoto ya wachezaji wanapotaka kuhama.

## M-Bet kuwagawia mashabiki zawadi

**Na Mwandishi Wetu**

Kampuni ya Michezo ya Kubahatisha ya M-Bet Tanzania, itaipamba fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kati ya Bayern Munich na Paris Saint- Germain kwa kutoa zawadi mbalimbali kwa mashabiki wa soka watakaojibu maswali mbalimbali.

Jumapili timu hizo zitakutana kwa mara ya kwanza kwenye fainali itakayopigwa Uwanja wa Ataturk Olympic, Uturuki wenye uwezo wa kuingiza watazamaji 76,092 na M-Bet imeandaa kumbi mbili, Samaki Samaki Mlimani City na Masaki ambapo watafunga 'screen kubwa' kwa ajili ya kuonyesha mpira huo.

Meneja Masoko wa Kampuni ya M-Bet Tanzania, Allen Mushi, alisema jana kuwa mbali ya kuendesha chemsha bongo inayolenga mechi hiyo na historia ya mashindano ya Champions League, pia burudani mbalimbali zitakuwapo kwa ajili ya kuburudisha mashabiki.

"Hii ni moja ya mikakati ya M-Bet Tanzania kuwakutanisha mashabiki pamoja na kujumuika kuangalia fainali hiyo ambapo zawadi kama za mipira, jezi, fulana na nyinginezo nyingi zitatolewa kwa watakaojibu maswali ya fainali ya mechi hiyo na historia ya Ligi ya Mabingwa ya Ulaya," alisema Mushi.

Alisema pia kutakuwa na maswali yahusiyo kampuni yao ambayo imefanikiwa kutoa washindi wengi na kuwazawadia zawadi mbalimbali ambazo zimeweza kubadili maisha yao.

## KVZ, Tekeleza fainali FA kesho

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

FAINALI ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) maarufu FA Cup, linatarajiwa kupigwa kesho katika Uwanja wa Gombani Kisiwani Pemba.

Mshindi wa fainali hiyo itakayozikutanisha KVZ kutoka Unguja na Tekeleza ya Kisiwani Pemba, ataiwakilisha Zanzibar katika michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, CAF.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Kamati ya Mashindano ya ZFF, Hussein Ahmada Vuai, alisema maandalizi ya kuelekea fainali hiyo kwa upande wa timu tayari yamekamilika ikiwamo KVZ tayari imesafiri kuelekea Pemba.

Alisema Kamati ya Mashindano kwa sasa ipo katika hatua ya mwisho ya kukamilisha maandalizi mengine ambayo yatahitajika katika fainali hiyo ili iweze kufanyika kama ilivyopangwa.

Michuano hiyo ya Kombe la FA, msimu huu kwa Unguja ilishiriki jumla ya timu 36, huku kwa Pemba ikishirikisha timu 38.

Michezo
Ijumaa Agosti 21, 2020
Nipashe



HABARI UK 22

Lewandowski na rekodi UEFA

KIFALME...



Mashabiki wa Yanga wakiwa wamembeba kwa kiti maalum, Mkurugenzi wa Uwekezaji wa GSM, Mhandisi Hersi Said, wadhamini wa klabu hiyo, baada ya kuwasili Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana akitokea DR Congo pamoja na wachezaji wawili, wanaonekana kwenye picha ndogo (juu kushoto) Mukoko Tonombe (anayepunga mkono) na Tuisila Kisinda, aliowasajiliwa kutoka Klabu ya AS Vita. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# YANGA YATETEMA DAR, MO, DIAMOND WATIKISA

## ●●● Senzo atambulishwa, bosi Simba amchambua akianika mazito, Mukoko, Kisinda watua na...

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU kongwe za soka nchini, Simba na Yanga, jana zilitetemesha Jiji la Dar es Salaam kwa muda baada ya kupokezana katika matukio mawili tofauti kuelekea maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu Bara 2020/21.

Mapema asubuhi, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Mohammed "Mo" Dewji akishirikiana na msanii wa muziki, Diamond Platinumz walizindua wimbo maalum wa klabu hiyo, ambao utapigwa katika Tamasha la Simba maarufu Simba Day, Jumamosi wiki katika Uwanja wa Mkapa.

Lakini baadaye, mashabiki wa Yanga walitetemesha jiji katika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere wakati wakimpokea Mkurugenzi wa Uwekezaji wa GSM, Injinia Hersi Said, ambao wanadhamini wa klabu hiyo, ambaye alitua akitokea DR Congo pamoja na wachezaji wawili, Mukoko Tonombe na winga Tuisila Kisinda, waliosajiliwa kutoka Klabu ya AS Vita.

**MO AFUNGUKA**

Akizungumza kuelekea tamasha la Simba Day, Mo alisema si la kukosa kwa kuwa mbali na Diamond, ambaye atakuwa mara yake ya kwanza kutumbuiza katika tamasha hilo, kutakuwa na wasanii wengine kibao na litakuwa la tofauti kabisa likitumia viwanja viwili wa Mkapa na Uhuru.

Aidha, Mo akizungumzia mikakati yake ndani ya klabu hiyo alisema ndani ya miezi mitatu wataanza ujenzi wa akademi ya klabu hiyo ambayo itakuwa ikilea vijana watakaolelewa kwa tamaduni za klabu hiyo ili kuwa na moyo wa kuitumikia.

Kuhusu kuondoka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Senzo Mazingisa ambaye alitambulishwa rasmi jana kuwa mtumishi mpya Klabu ya Yanga, Mo alisema anasikia kwamba ameondoka na baadhi ya nyaraka za Simba, lakini haziwezi kuwasaidia chochote na kuwataka Wanasimba kutulia muda si mrefu watampata mtu sahihi.

Alisema kuna changamoto nyingi ndani ya klabu hiyo na kwamba kuna baadhi ya watu wana maneno mengi, wengine wakitaka kubomoa, lakini kuondoka kwa Senzo hakuwezi kurejesha nyuma katika kuiendeleza klabu hiyo kuweza kufikia mafanikio.

"Senzo kawahi kuondoka wakati mwezi huu tulikuwa tufanye mkutano atupe mkakati wake ni namna gani tunaweza kuongeza mapato ya klabu na kupunguza matumizi, unajua tamasha kama hili la Simba Day, lilikuwapo kabla yake, hivyo tulikuwa tunataka kujua vyanzo vipya vya mapato kutoka kwake, lakini naona katuwahi.

"Muda si mrefu tutamtangaza CEO mpya ambaye atakuwa na uchungu na klabu hii, bora tumpeleka hata Uswisi kusoma ili aweze kuitumikia klabu yetu kwa moyo," alisema.

Mo pia alisema klabu hiyo haitakubali kuuza mchezaji yeyote kwa sasa licha ya baadhi ya timu kutoka nje ikiwamo Uswisi awali kuweka dola 500,000 mezani wakimtaka Luis Miquissone, lakini walikataa.

Alipoulizwa kuhusu Sh. bilioni 20 za uwekezaji, alisema: "Unajua huu muundo mpya wa uwekezaji ni mgeni hapa kwetu, lakini tupo katika hatua za mwisho kukamilisha baadhi ya mambo, kama mnafuatilia mimi kwa utajiri wangu nashindwa kutoa kiasi kama hicho? Hizo fedha zipo.

"Ukiacha hizo bilioni 20, lakini kwa sasa tambua natoa Sh. bilioni 3 kwa mwaka kusaidia baadhi ya shughuli nyingine klabu ikiwamo mishahara ya wachezaji."

Kuhusu kikosi kilichosajiliwa msimu huu, alisema wapo wanaowabeza wakidai ni wachezaji waliomaliza mikataba yao na hawana uwezo, lakini hana shaka katika hilo kwa kuwa hata baadhi ya makocha maarufu akiwamo Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Zambia, Milutin Sredojevic 'Micho', amekiri ubora wa nyota waliowasajili, Larry Bwalya na Chris Mugalu.

Kwa upande wa Diamond, ambaye alishusha mistari ya wimbo huo maalum na kucheza sambamba na Mo, aliweka wazi yeye ni shabiki wa Simba na kuwataka kuhudhuria Uwanja wa Mkapa Jumamosi kumshuhudia akifanya makubwa.

**MAPOKEZI YANGA**

Katika mapokezi ya Yanga, jana mashabiki walimpokea kwa mbwembwe tajiri wa klabu hiyo, Hersi kwa kumbeba kama Sultan ama Mfalme, akiwa amekaa katika kiti kilichobebwa juu kwa juu, wakifurahi kwa kukamilisha usajili wa nyota hao wawili.

Hata hivyo, hawakufika mbali kabla ya kumshusha na kupanda gari kisha kuelekea klabuni ulipofanyika utambulisho wa wachezaji hao kabla ya kuondoka kwenda kupumzika.

Lakini mashabiki walikosa fursa ya kusalimiana na nyota hao, Kisinda na Mukoko kutokana na mvutano uliojitokeza katika Uwanja wa Ndege wa namna ya kuwapokea, hivyo wakapandishwa kwenye gari na kuelekea moja kwa moja klabuni ambapo walitambulishwa.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema, wachezaji hao wataanza kuonekana leo katika mazoezi ya timu hiyo yanayoendelea kwenye Uwanja wa Chuo cha Sheria jijini Dar es Salaam.

"Kesho (leo) wataungana na wenzao katika mazoezi, hivyo Wanyanga wasubiri mambo mazuri," alisema.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042